SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 2

## Ripoti ya samaki waliokufa Mto Mara yatolewa






UKURASA 9

Nipashe Jumapili
MWANGA WA JAMII
Jumapili Machi 13, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580883
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# KUMEKUCHA

## **Harufu** mikutano vyama vya siasa yanukia, Rais aagiza kanuni zitungwe, CHADEMA, wasomi watoa ya moyoni...

*Endelea ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Wajumbe wa Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. Wa (tatu kushoto) ni Mwenyekiti wa Kikosi Kazi hicho, Prof. Rwekaza Mukandala na (wa nne kushoto) ni Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe. **PICHA: IKULU**

## CCM yaitaka serikali ichukue hatua mwenendo Jeshi la Polisi

UKURASA 3

## GSM amjibu rasmi Makonda, amtaka wakutane kortini



UKURASA 3



Mwanasheria Alex Mgongolwa, akiwaonyesha waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, moja ya vielelezo alivyonavyo vya umiliki wa kiwanja namba 60 chenye hati namba 186153/60 kilichopo eneo la Regent, Manispaa ya Kinondoni, mali ya mteja wake, Gharib Said Mohamed (GSM). **Picha ndogo:** Moja ya nyaraka alizozionyesha. **PICHA: ROMANA MALLYA**

MICHEZO SIMBA YAKAMILISHA RAMANI YA USHINDI UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Ripoti samaki kufa Mto Mara yatolewa

**Na Richard Makore,** MWANZA

SIKU nne baada ya samaki aina ya sato kuonekana wakielea wakiwa wamekufa ndani ya Mto Mara mkoani Mara, Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria imetoa matokeo ya utafiti wa sampuli za maji waliyopima katika maabara yao.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha samaki hao wamekufa kutokana na kukosa hewa ya oksijeni kutokana na kuwapo mafuta aina ya oili na grisi yaliyotanda juu ya maji eneo la Mto Kirumi.

Mwanzoni mwa mwezi huu, samaki walionekana wakielea huku wakiwa wamekufa katika mto huo na kuzua taharuki kwa watu wanaopakana na eneo hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Mwanza, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinhu, alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwapo kiwango kikubwa cha mafuta aina ya oili na grisi.

Alisema katika maji hayo wamebaini kuwapo kiwango kikubwa cha mafuta hayo kuliko kinachokubalika kwa mujibu wa viwango vya ubora wa maji Tanzania cha TZs 2068:2017.

Shinhu alisema kukosekana kwa hewa ya oksijeni ndani ya maji kumesababisha vifo vya viumbe hai wakiwamo samaki.

Kuhusu maji kuwa meusi na kutoa harufu mbaya, mkurugenzi huyo alisema wanaendelea na uchunguzi ili kubaini hali hiyo imetokana na nini.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo hakusema yalikotoka mafuta hayo yaliyotanda juu ya maji kwenye mto huo, zaidi ya kubainisha kuwa chini ya Daraja la Kirumi kumetanda mafuta hayo, akisisitiza bado wanaendelea na uchunguzi.

Habari kutoka katika vijiji vinavyopakana na mto huo, zinadai wananchi ambao wanatumia maji hayo kwa ajili ya kunywa, kunywesha mifugo na kufanya shughuli za uvuvi, wameingiwa hofu.

Licha ya samaki hao kufa wenyewe, baadhi ya wananchi wametumia fursa hiyo na kuingia mtoni na kuwaokota kisha kuwauza kwa wananchi kwa bei rahisi.

Vijiji vilivyokumbwa na tatizo hilo ni pamoja na Kuruya, Kwibuse na Marasibora na maji hayo yaliyochufuliwa yanaingia katika Ziwa Victoria, jambo ambalo linaweza kusababisha samaki zaidi kufa ziwani.

Akizungumzia sakata hilo siku nne zilizopita, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rashid Tamutamu, alisema uchunguzi wa vifo hivyo vya samaki umeanza.

Alisema sampuli za samaki hao zimepelekwa katika maabara ya usalama wa chakula mjini Musoma mkoani Mara ili kujua chanzo cha vifo hivyo.



Wakazi wa Kijiji cha Barakiwa, Wilayani Liwale, mkoani Lindi, wakishuhudia daraja la Ndunyungu, lililoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha lisipitike. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kumekucha mikutano vyama vya siasa

**Augusta Njoji na Paul Mabeja,** DODOMA

KUMEKUCHA. Ndivyo ambavyo inaweza kuelezwa kutokana na kuwapo kwa nuru ya kuanza rasmi kufanyika kwa mikutano ya vyama vya siasa ambayo haikuwapo kwa zaidi ya miaka sita sasa.

Dalili hizo zinatokana na agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kumwagiza Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, kuandaa kanuni zitakazoelekeza jinsi ya kufanya mikutano ya hadhara ya vyama hivyo.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana alipokuwa akipokea maazimio ya awali kutoka kikosi kazi alichokiteua chenye wajumbe 24 cha kufuatilia hoja zilizojitokeza kwenye Mkutano wa Wadau wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa, uliofanyika Desemba 15 hadi 17, mwaka jana, jijini hapa.

Alimwagiza kuwa uandaaji wa kanuni hizo ushirikishe Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) na Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS).

**MAAZIMIO KIKOSI KAZI**

Katika taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, kikosi kazi hicho kiliwasilisha maazimio yaliyogawanyika katika makundi matatu ya muda na utekelezaji.

Yunus alisema muda mfupi ni uandaaji wa kanuni zitakazoelekeza jinsi ya kufanya mikutano ya hadhara ya vyama hivyo.

Pia alisema baadhi ya maazimio ya muda wa kati ni pamoja na rushwa na maadili katika uchaguzi, ruzuku na elimu ya uraia huku masuala yanayohusu uchaguzi na katiba mpya vikiwa ni mpango wa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Kuratibu Maoni ya Wadau wa Demokrasia, Prof. Rwekaza Mukandala, alisema: "Leo (jana) tulikuwa tunamweleza Rais tumefika wapi na kumpa mrejesho huko tunakotaka kwenda na hii kazi na kumpa mrejesho unaostahili."

Alisema kazi bado haijakamilika ndiyo imeanza na hayo ni mapendekezo ya awali waliyowasilisha ambayo yamepokewa na Rais kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

**MAONI YA WADAU**

Akitoa maoni kuhusu uandaaji wa kanuni hizo, Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Catherine Ruge, alisema: "Jambo linalonishangaza ni kwamba tunaendaje kutunga kanuni wakati tuna Katiba ambayo inaelezea kuhusu mikutano ya hadhara?

"Tuna Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019. Habari ya mikutano ya vyama vya siasa imeelezwa lakini pia ina kanuni zake. Wakati nikiwa bungeni nilishiriki kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Nashindwa kuelewa wanakwenda kutunga kanuni zipi, labda iwe ni kuzipitia na kufanya marekebisho au wanaenda kutunga nini? Labda maadili ya mikutano ya vyama vya siasa lakini kuhusu kanuni ya sheria ya vyama vya siasa inaonyesha mikutano ifanyikaje na wajibu wa vyama vya siasa kufanya mikutano.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Tanzania Bara, Benson Kigaila, alisema: "Kwanza sisi siyo watu sahihi wa kutoa maoni yetu juu ya suala hilo kwa sababu hatukushiriki katika kikao cha kwanza. Lakini kwa mtizamo wangu nadhani hakuna haja kwa sababu sheria ya vyama vya siasa ipo tangu mwaka 1992 na kanuni zake zipo."

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema wanafarijika suala la mikutano limepewa uzito na inapaswa kufunguliwa mapema.

"Hili ni jambo jema. Rai yetu juu ya hilo ni kwamba kanuni zinazotungwa wahakikishe haziwi kikwazo bali ziweke mazingira rahisi kwa sababu sheria inatupa uhuru wa kufanya mikutano lakini mara nyingi Jeshi la Polisi limekuwa likitumia utaratibu wa kupeleka taarifa ya mikutano ya hadhara wanabadili inakuwa kuomba kibali cha mikutano ya hadhara," alisema.

Hata hivyo, aliomba suala la Tume Huru ya Uchaguzi lifanyiwe kazi kwa haraka kwa kurekebisha sheria ya uchaguzi ili kuwa na tume ambayo itafanikisha uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024 na uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Naye Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Paul Loisulie, alisema utengenezaji wa kanuni hizo utafungua milango ya kujenga utaratibu wa kudumu wa kuendesha shughuli za siasa kwa ujumla.

"Jambo la msingi kuhusu agizo la mikutano ya hadhara ni ushirikishwaji wa wadau wote husika ili upatikane utaratibu wenye maridhiano. Si vizuri utaratibu ukatengenezwa halafu wengine wakaupinga. Tutakuwa hatujafanikiwa kwa kile tunachokusudia," alisema.

## HABARI KITAIFA



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu chama hicho, kuandaa mdahalo wa kuazimisha miaka 100 ya kuzaliwa kwa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# GSM amtaka Makonda apeleke mgogoro kortini

**Na Romana Mallya**

MWANASHERIA Alex Mgongolwa amesema mteja wake, Gharib Said Mohamed, maarufu GSM, ndiye mmiliki halali wa kiwanja namba 60 chenye hati namba 186153/60 kilichoko Regent Estate wilayani Kinondoni na kumtaka yeyote mwenye vielelezo vya umiliki mwingine, aende ngazi yoyote ya kisheria.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam na waandishi wa habari, Mgongolwa alisema mteja wao amewapa maelekezo mawili, ikiwamo kuchukua hatua zote za kisheria dhidi ya mtu yeyote anayefanya upotoshaji kuhusu umiliki na uendelezaji wa eneo hilo.

"Tunampa changamoto mtu yeyote anayedhani kwamba ana hati yoyote ya umiliki kuleta vielelezo vyake hadharani au katika mamlaka zinazohusika pale atakapoona inafaa, tupo radhi kwenda kuthibitisha vinginevyo kwa mujibu wa vielelezo tulivyonavyo," alisema.

Pia alisema mteja wao amewapa maelekezo ya kutumia sheria zote za nchi kulinda heshima yake aliyojijengea kibiashara ndani na nje ya nchi.

"Kwa kuwa tukio ni moja lililotokea, hatua ambazo tutazichukua kuanzia sasa zitategemea matukio yatakayofuata.

Matukio yatakayofuata ndiyo yatakayotupa mwongozo wa nini cha kufanya. Ikitokea hatua ya kwenda mahakamani tutakwenda, ikitokea hatua ya kuangalia kama kuna ngazi yoyote ambayo tunatakiwa kulipeleka, tutalipeleka," alisema.

Kuhusu video fupi iliyosambaa mtandaoni hivi karibuni ikimwonyesha Paul Makonda (aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam) akiwa kwenye jengo linaloendelea na ujenzi huku akilalamika, Mgongolwa alisema kuwa baada ya kupewa kilichotokea waliombwa watoe ushauri.

"Tuliombwa tutoe ushauri kwa mazingira yake na mazingira yale yanatafsirika kisheria kwamba ni mtu anataka kuzungumzia umiliki wenza kwenye lile eneo.

"Ushauri wetu ni dhahiri kwamba umiliki wa ardhi ni umiliki unaotolewa na mamlaka husika. Kwa hiyo, ukienda kwenye mamlaka husika ikakuonyesha kwamba mmiliki wa ardhi mfano ni Alex Mgongolwa, basi sheria inasema huo ni ushahidi wa kutosha kwamba huyo ndiye mmiliki.

"Baada ya kujiridhisha na hilo kwamba yeyote ambaye anadhani ana haki ya eneo hilo, sisi hiyo haki hatujaiona katika mamlaka husika kwa mujibu wa sheria.

"Kama unamiliki ardhi na kuna mtu mwingine ana haki kwenye ile ardhi haki hiyo ya mtu wa tatu, huwa inaweza kufanyiwa usajili pale Ardhi.

"Tunachokipata kwenye sheria ni kwamba huyu (GSM) ni mmiliki huru katika eneo hili kwa mujibu wa sheria za nchi."

Katika mkutano huo, Mgongolwa alionyesha vielelezo alivyoviita ni vya kihalali kisheria ambavyo alisema ni nakala halisi zinazoonyesha umiliki halali wa mteja wake katika eneo hilo.

"Mteja wangu alinunua ardhi hii kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi Novemba 21, 2006, hiki ni kielelezo namba moja na kimetoka mamlaka zinazohusika na mimi na mteja wangu tulikwenda kudhibitisha Wizara ya Ardhi nayo ilidhibitisha mmiliki wa kiwanja hiki mpaka sasa ni Ghalibu Saidi Mohamed.

"Baada ya kumiliki kiwanja mteja wangu alifuata hatua zote ili kufanya mwendelezo wa kiwanja na Septemba 19, 2017 aliingia mkataba na kampuni ya ujenzi kwa gharama ya Sh. milioni 640," alidai.

Mgongolwa alisema wakati anataka kuanza ujenzi alifuata utaratibu wa kupata kibali maalumu cha ujenzi katika Manispaa ya Kinondoni na maombi yalijibiwa Oktoba 16, 2017 na kilitoka kwa jina lake kikiwa na namba 00020032.

# Dereva wa bajaj adaiwa kuuawa kisa chenji 400/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limemkamata mfanyabiashara mdogo katika Mtaa wa Tofiki, Kata ya Viwandani jijini Dodoma, akituhumiwa kumuua dereva bajaj kisa chenji ya Sh. 400 aliyokuwa akimdai baada ya kutoa Sh. 500 kununua sigara.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema tukio hilo lilitokea Machi 8, mwaka huu.

Mtuhumiwa anadaiwa kumpiga nyuma ya shingo na kumsababishia kupoteza maisha dereva bajaj huyo kwa kipande cha bomba la chuma chenye urefu wa Sm 76 na upana wa Sm tatu.

Kamanda Lyanga alisema mtuhumiwa huyo na wengine wamefikishwa mahakamani kwa ajili ya kuendelea na taratibu zingine za kisheria.

Katika tukio lingine la mauaji lililotokea Mtaa wa Mtumba mkoani hapa, Jeshi la Polisi limeopoa kwenye mtaro mwili wa mwanamke anayesadikiwa kuwa na umri wa miaka 40. Kamanda Lyanga alisema baada ya uchunguzi wa daktari, inaonyesha mwanamke huyo alikabwa na kubakwa na wahalifu.

Alisema jeshi hilo pia Machi 4, mwaka huu lilikamata nyara za serikali (pembe za ndovu) vipande vinne kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori katika nyumba ya kulala wageni iliyoko Kata ya Mtera, Tarafa ya Rudi wilayani Mpwapwa. Alisema vipande hivyo vyenye uzito wa kilogramu 10, vina thamani ya Sh. milioni 69. Pia alisema askari wa jeshi hilo waliokuwa katika doria wamekamata pikipiki ikiwa imebeba viroba viwili vya salfeti vilivyokuwa na bangi.

Alisema kuwa Machi 9, mwaka huu, Jeshi la Polisi pia lilikamata watuhumiwa wanne katika Kijiji cha Mbande, Kata ya Sejeli wilayani Kongwa, wakiwa kwenye gari aina ya Toyota RAV 4 yenye namba IT 8209, wakidaiwa kuwa na mabegi mawili yenye bangi kilo 10 iliyokuwa ikisafirishwa.

Mbali na hilo, pia wamemkamata raia wa Rwanda (34) ambaye ni Mtusi na mjasiriamali akiwa ameingia nchini bila kibali chochote, pia mwanamke (54), raia wa Burundi anayedaiwa kuingia nchini bila kibali.

Kamanda Lyanga alisema jeshi hilo linawashikilia watuhumiwa wengine 10 kwa tuhuma za wizi wa pikipiki katika maeneo mbalimbali jijini Dodoma.

Kamanda alisema kwa upande wa makosa ya barabarani kuanzia Februari hadi sasa, kuna makosa 6,478 ambayo faini zake zimewezesha kupatikana Sh. milioni 198.

# CCM yataka hatua mwenendo wa Polisi

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema Kamati Kuu ya chama imejadili na kupitisha mapendekezo ya marekebisho ya Katiba ya chama hicho ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2020 kwa lengo la kuongeza kasi na ufanisi wa kazi za chama na utekelezaji wa uamuzi wa vikao vya chama.

Vilevile, chama hicho kimeelekeza serikali kuangalia upya mwenendo wa Jeshi la Polisi nchini ambao umekuwa hauridhishi na kulalamikiwa na wananchi.

Shaka aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri ya CCM kilichofanyika juzi chini ya Mwenyekiti, Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dodoma. Alisema lengo kuu la maboresho hayo ni kukiwezesha chama kupata viongozi imara, waadilifu na wenye uwezo mkubwa katika kuongoza na kusimamia majukumu ya serikali za mitaa kwa ufanisi.

"Marekebisho yanalenga kuongeza na kuimarisha udhibiti wa chama kwa viongozi wake wanaochaguliwa kuongoza na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM kupitia serikali za mitaa," alisema Shaka. Pia alisema marekebisho yanakusudia kuimarisha nguvu za chama katika kukabiliana na kudhibiti vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. "Kuongeza uwakilishi wa jumuiya za CCM ngazi ya kata kwenye Mkutano Mkuu wa CCM wa wilaya na kurekebisha itifaki ya uwakilishi unaofanana wa wenyeviti na makatibu wa jumuiya za CCM wa ngazi ya mkoa kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na wa ngazi ya wilaya kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa," alisema.

Shaka alisema kwa mujibu katiba ya CCM, mamlaka ya kupitisha na kurekebisha Katiba ya chama yapo mikononi mwa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa.

Alisema Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa imeazimia kuwasilisha kwa Halmashauri Kuu ya CCM taifa pendekezo la kuitishwa kwa Mkutano Mkuu Maalum.

Alisema Machi 31 mwaka huu, Kamati Kuu ya CCM itakutana na kufuatiwa na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa siku hiyo hiyo.

Shaka alisema kuwa Aprili 1 mwaka huu, Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa utafanyika na vikao vyote vilivyotajwa vitafanyika Makao Makuu ya CCM Dodoma. Shaka pia alisema Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa imepitisha mpango wa chama hicho kuhusu maadhimisho ya kumbukizi ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Shaka alisema kwa mwaka huu wataadhimisha kumbukizi ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa kiongozi huyo mahiri, mzalendo na mwanamapinduzi wa kweli ambaye kifo chake kilitangazwa Oktoba 14, 1999.

Shaka pia alisema Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa imempongeza Rais Samia kwa uamuzi wake wa kuunda tume kufuatilia matukio mbalimbali ya uhalifu na kusababisha baadhi ya Watanzania kuuawa katika mikoa ya Mtwara na Tanga. Alisema Kamati Kuu imeelekeza serikali kuangalia upya mwenendo wa Jeshi la Polisi nchini ambao umekuwa hauridhishi na kulalamikiwa na wananchi kutokana na matendo yanayofanywa na baadhi ya maofisa na askari wa jeshi hilo kinyume cha mwongozo na utendaji kazi wa jeshi hilo.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU BARUANI MOHAMED AKILIMALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la **MAXAM AGENCY CO.TD** aina ya **HONDA** yenye namba za usajili **T215BLD.**Engine **No. MD17E3007172.** Chassis No. **MD221007155.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/101676/2022.**



**JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.**

DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING

HEAD OFFICE -Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza, Tarime, Geita, Musoma, Bukoba

P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040, josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Amri tuliyopewa na Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya ya Bukoba. **JOSINA COMPANY LIMITED,** Itaendesha mnada wa hadhara wa kuuza Eneo la Kanisa lililopo katika kitongoji cha Biyungu,kijiji cha Kiruruma, wilaya ya Karagwe.hii ni kutokana na shauri la madai namba 303/2021 kati ya **THE RIGISTERED TRUSTEES OF PONTECOSTAL HOLINESS CHURCH WITHOUT DANCE DHIDI YA THE REGISTERED PONTECOSTAL HOLINES MISSION.**

**Mnada huu utafanyika tarehe 21/03/2022,siku ya juma tatu.**

**MASHARTI YA MNADA**

**ENEO/KANISA** litauzwa kama lilivyo ,mnunuzi atalipia 25%ya bei yam nada papo hapo baada ya nyundo ya dalali na 75%italipwa ndani ya siku kumi na nne (14)toka siku ya mnada ,na akishindwa kulipa mnada utarudiwa na pesa iliyolipwa awali haitarudishwa.

Ukaguzi wa eneo hilo la kanisa utaanza siku ya t**arehe 19/03/2022.**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia namba 0713203040** *116748102*

MAKALA MAALUM

## MWAKA MMOJA WA SAMIA IKULU

# Neema yashuhudiwa Sekta ya Kilimo

## ■Tanzania yajenga maghala nchi jirani
## ■Mikataba 17 yatiwa saini Dubai Expo



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia) akitia saini moja ya mikataba wakati Rais Samia Suluhu Hassan alipokwenda Dubai na baadhi ya viongozi waandamizi wa serikali kutangaza fursa za uwekezaji nchini hivi karibuni. Tanzania iliingia makubaliano ya mikataba 30. Kati yake, 17 ni ya Sekta ya Kilimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOZUNGUMZIA kilimo, unaitaja sekta inayochangia asilimia 26.9 kwenye Pato la Taifa, kwa mujibu wa taarifa za mwaka 2020 za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Unakuwa umeigusa sekta inayochangia asilimia 100 ya mahitaji ya ndani ya chakula; inayoajiri zaidi ya asilimia 61.5 ya Watanzania; inayochangia asilimia 65 ya malighafi viwandani.

Pia unakuwa umeitaja sekta inayochangia mapato ya fedha za kigeni wastani ya Dola za Marekani bilioni 1.2 kwa mwaka; bila kusahau takriban asilimia 59 ya mwenendo wa mfumuko wa bei nchini hutegemea hali ya uzalishaji katika kilimo.

Kwa kutambua umuhimu wake, Rais Samia Suluhu Hassan katika mwaka wake wa kwanza madarakani, haijaiacha nyuma Sekta ya Kilimo.

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Ikulu, serikali imezipatia Wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) jumla ya Sh. bilioni 129 kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya nafaka ambayo yatauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Bashe pia anasema serikali imeongeza bajeti ya utafiti kutoka Sh. bilioni 7.35 hadi Sh. bilioni 11.63, huduma za ugani kutoka Sh. milioni 603 hadi Sh. bilioni 11.5, umwagiliaji kutoka Sh. bilioni 17.7 hadi Sh. bilioni 51.48, uzalishaji wa mbegu kutoka Sh. bilioni 5.42 hadi Sh. bilioni 10.58.

"Sh. bilioni 3.63 zimetolewa kwa ajili ya kuwezesha TARI, TORITA, TRIT, TPHPA na TACRI kufanya utafiti wa mazao ya kilimo ikiwamo mchikichi, zabibu, mkonge, ngano, alizeti, kahawa, chai na tumbaku.

"Tathmini ya mahitaji ya ukarabati wa maabara inafanyika ili kuimarisha uwezo wake na kupata ithibati ambapo tayari maabara moja ya TPHPA imepata ithibati.

"Pikipiki 250 zimenunuliwa na Bodi ya Pamba na kuzigawa kwa maofisa ugani katika mikoa ya Mara, Geita, Kigoma, Mwanza na Shinyanga. Taratibu za ununuzi wa pikipiki 2,000 zipo hatua za mwisho za kutia saini mkataba.

"Taratibu za ununuzi wa simu janja 384 zimekamilika na mzabuni ameshasaini mkataba; ununuzi wa Extension kits 3,483 (Sprayers, Gumboots & Overcoats) umefanyika na vifaa vimeanza kusambazwa.

"Taratibu za ununuzi wa vifaa 143 vya kupima afya ya udongo (Agrocares Scanner) zimekamilika na taratibu za kuhakiki ubora zinakamilishwa," Bashe anafafanua.

Waziri huyo anataja mafanikio mengine katika mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani ni kufungua masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwamo soko la parachichi (India na Afrika Kusini) na ndizi (Kenya) baada ya kukidhi viwango vya ubora.

Anasema CPB imefungua vituo vya mauzo katika miji ya Juba (Sudan Kusini) na Lubumbashi (DRC) na kukodi maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 na 2,000 mtawalia.

Anabainisha kuwa NFRA wamenunua tani 110,516.717 za mahindi na hivyo kuwa na akiba ya tani 214,000 za nafaka katika maghala yake huku serikali ikifanikisha uuzaji wa soya nje ya nchi kufikia tani 53,594.35 mwaka 2020/21 kulinganishwa na tani 2,647 mwaka 2019/20.

"Kampuni 80 za Kitanzania zimesajiliwa kuuza soya China. Wizara imesaini Hati ya Makubaliano ya miaka mitano na Kampuni ya Smart Import and Export ya Misri kwa ajili ya ununuzi wa mahindi ya njano na rasimu ya makubaliano ya kuuzia India mazao ya jamii ya mikunde, hususan mbaazi, imeandaliwa na taratibu zinaendelea," Bashe anasema.

Anaendelea: "Pia tumefanikiwa kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji vibali na usafirishaji wa mazao (Agriculture Trade Management Information System -ATMIS).

"CPB imeingia mkataba na wakulima 264 za zao la ngano (Siha, Karatu, Monduli na Hangang') ambao wamewezeshwa mbegu bora tani 210. CPB imeingia mkataba na Grain Industries Ltd ya Kenya kuiuzia tani 144,000 za mahindi. Hadi Novemba CPB imeuza tani 2,000.

"NFRA imeingia mkataba na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tani 3,600 za mahindi. Pia imeingia mkataba na Grain Industries Ltd kuiuzia tani 5,000 mahindi.

"Mikopo ya Sekta ya Kilimo imeongezeka kutoka Sh. trilioni 1.9 mwaka 2020/21 mpaka Sh. trilioni 2.4 mwaka 2021/22 kati ya mikopo yote ambayo ni Sh. trilioni 20 kwa mwaka," anafafanua.

Bashe anataja malengo ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha (2022/23), yakijumuisha ukuaji wa Sekta ya Kilimo kutoka asilimia tano hadi kufikia asilimia 6.1 ifikapo mwaka 2025 (FYDP III); ukuaji wa sekta ndogo ya mazao kutoka asilimia 4.1 mwaka 2019/20 hadi 5.7 mwaka 2025/26 na mauzo ya mazao nje ya nchi kuongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.2 hadi kufikia Dola bilioni tano ifikapo mwaka 2025.

Anataja lengo lingine ni kuongeza uzalishaji kwa mazao ya chakula kwa asilimia 136 kutosheleza idadi ya watu milioni 135 ifikapo 2050.

Waziri pia anaainisha malengo ya serikali katika uzalishaji wa mazao yanayojumuisha: Kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kutoka tani 300,000 hadi tani 700,000 ifikapo 2025; kuongeza uzalishaji wa pamba kutoka tani 350,000 hadi kufika tani 1,000,000 ifikapo 2025.

Mengine ni kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 68,000 hadi kufikia tani 300,000 ifikapo 2025; kuongeza uzalishaji wa majani ya chai kutoka tani 37,000 za sasa hadi tani 60,000 ifikapo 2025; kuongeza uzalishaji wa tumbaku kutoka tani 60,595 hadi tani 200,000 ifikapo 2025; kuongeza uzalishaji pareto kutoka tani 2,400 hadi tani 3,200 ifikapo 2025; na kuongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 38,506 hadi tani 80,000 ifikapo 2025.

"Wizara imejipanga kuhakikisha Tanzania inajitosheleza kwa mahitaji ya chakula ndani ya nchi na kuuza ziada nje ya nchi. Pia kufanya mwelekeo wa Sekta ya Mazao ya Chakula kuwa wa kibiashara.

"Pia tumejipanga kuongeza ushiriki wa vijana kujiajiri katika Sekta ya Kilimo ikiwamo kuanzisha miradi itakayoshawishi vijana kujiajiri katika sekta ya kilimo.

"Tunalenga kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwenye viwanda vya kuongeza thamani kutoka asilimia 65 za sasa kufikia asilimia 100 ifikapo 2025," anasema.

Waziri Bashe pia anasema wizara inalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta ya kula ili kujitosheleza na kufidia uhaba uliopo na kuuza ziada nje ya nchi.

Pia kuongeza mauzo ya Sekta ndogo ya Horticulture kutoka Dola milioni 750 kwa mwaka kufikia Dola bilioni mbili kila mwaka kuanzia mwaka 2030.

Vilevike, kuongeza huduma za utafiti wa mbegu bora katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za wakulima; kufanya huduma ya upimaji wa afya ya udongo kuwa huduma muhimu kwa wakulima na huduma hiyo ipatikane bure kwa wakulima wadogo.

"Pia tunalenga uanzisha mfuko wa ruzuku wa pembejeo na mazao; ujenzi wa miundombinu muhimu katika Sekta ya Kilimo, ikiwa ni pamoja na maghala katika ngazi ya kijiji, kata na tarafa ili kuondoa tatizo la post-harvest loss kufikia single digit ifikapo 2030.

"Vilevile, tunalenga kuendelea kufungua maghala katika nchi zenye masoko makubwa ikiwamo Vietnam, China na Saudi Arabia. Kati ya mikataba 30 iliyotiwa saini Dubai Expo, 17 ni ya Sekta Kilimo," Bashe anahitimisha.

## HABARI KITAIFA

# Ufugaji funza fursa wanufaika TASAF

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa majaribio wa funza uliobuniwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umetajwa kuibua fursa kwa wanufaika wa mfuko huo katika Halmashauri ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Mratibu na Msimamizi wa TASAF Kinondoni, Balima Mpinga na Teddy Kyala, walisema funza hao wanaozalishwa na nzi aina ya nzi chuma, hutumika kama chakula cha mifugo kama kuku, nguruwe na samaki.

Walisema kwa sasa mradi huo umevutia wanufaika wa TASAF na wananchi wengine ambao wameonyesha nia ya kujikita katika shughuli hiyo ya uvunaji wa funza hao.

"Kwa sasa funza hao ni gumzo kubwa jijini kutokana na jinsi wanavyozaliana kwa njia rahisi ya mabaki ya vyakula kutoka majumbani," alisema Kyala.

Kyala alisema kuwa kwa sasa mradi huo unaetekelezwa na kikundi kimoja cha wanufaika wa TASAF Kinondoni wakisimamia na kuendelea kufanya utafiti wa kuboresha mradi huo.

Alisema kuwa funza hao walikuwa wakivutia wafugaji wa mifugo baada ya kugundua kuwa walikuwa chakula chenye ubora mkubwa na kilikuwa hakina kemikali kama vyakula vingine vya mifugo.

Mpinga alisisitiza kufunguka kwa fursa kwa wanufaika hao kwa kuanzisha miradi yenye tija kama huo wa funza.

Aliwataka wanufaika kuangalia miradi kama ya ukulima wa uyoga, ufugaji wa samaki na uvunaji wa majongoo kama fursa nyingine kwa wanufaika hao.

Mpinga alisema kuwa ofisi yake ilikuwa na nia ya kuendelea kuanzisha miradi mingi ili wanufaika waibue fursa nyingi kujikita kwa ajili ya kundokana na umaskini.

Naye mvunaji wa funza hao, Stumai Ali Kapambila, alisema kuwa alikuwa akivuna funza wengi na kuweza kuwauza kwa wafugaji na kujipatia fedha.

Kapambila alisema kuwa kikundi chake kiliuza funza hao kwa bei ya Sh. 2,000 kwa kilo.

Hata hivyo, Kapambila alisema uvunaji mkubwa wa funza hao ulihitaji kiwango kikubwa cha mabaki ya vyakula kutoka majumbani ambayo kwa sasa hayatoshelezi.

Alisema kikundi chake kinachohudumia mradi huo hulazimika kununua mabaki ya vyakula kutoka kwa wenye migahawa na mamalishe.

Aisema kwa sasa wenye migahawa na mamalishe huuza kwa bei kubwa mabaki ya vyakula, jambo linalolazimisha upatikanaji mdogo wa mabaki ya vyakula kwa ajili ya uzalishaji mkubwa wa funza hao.

# MNH yapandikiza wagonjwa 11 uloto kwa milioni 770/-

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imetumia Sh. milioni 770 kwa wagonjwa 11 kupandikizwa uloto nchini, tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo Novemba mwaka jana, hivyo serikali kuokoa Sh. bilioni 1.98.

Taarifa iliyotolewa na MNH juzi, ilibainisha kuwa iwapo wagonjwa hao wangetibiwa nje ya nchi, serikali ingetumia Sh. bilioni 2.75 kwa gharama ya Sh. milioni 250 kwa mgonjwa mmoja.

Naibu Mkurugenzi wa MNH, Dk. Julieth Magandi, akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, alisema hivi sasa wagonjwa sita wanafanyiwa huduma hiyo kila mwezi kuanzia Februari mwaka huu, kutokana na kuwapo wataalamu na miundombinu.

"Fedha zilizotolewa na serikali ni Sh. bilioni 6.2 kuwezesha uanzishwaji wa huduma hii. Wagonjwa wanaopandikizwa uloto ambao wana matatizo ya saratani ya damu (multiple myeloma na lymphoma).

"Huduma hii pia hutolewa kwa wagonjwa wenye saratani mbalimbali za damu pamoja na wenye selimundu.

Mgonjwa wa aina hii akienda nje ya nchi gharama yake ni kati ya Sh. milioni 200 hadi milioni 250. Huduma hii sasa inafanyika hapa nchini kwa wastani wa Sh. milioni 70 kwa mgonjwa," alisema Dk. Magandi.

Alisema Tanzania inakuwa nchi ya kwanza kutoa huduma hiyo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, pia nchi ya sita barani Afrika na imekuwa endelevu. "Umri wa waliopandikizwa uloto ulikuwa ni chini ya miaka 60 sasa tunatoa huduma hata kwa zaidi ya umri huo, tumeongeza aina nyingine ya saratani ya damu inayohusisha matezi (Lymphoma)."

Septemba mwaka jana, MNH ilinunua mashine mbili maalum aina ya Spectra Optia, zenye thamani ya Sh. milioni 245 ili kuisaidia kutoa tiba kwa magonjwa 10 ikiwamo kupandikiza uloto.

# Polisi yatenga siku maalum utatuzi migogoro ya ndoa




**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani hapa limetenga siku maalumu kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya kifamilia ikiwamo ya ndoa, hatua ambayo tangu kuanzishwa, imetatua migogoro 10 ya wanandoa katika kipindi cha wiki mbili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilim (pichani), alisema hayo juzi wakati akizungumza na kinamama kwenye banda la maonyesho la Ngaiza Foundation wakati wa maadhimisho ya sherehe za wanawake yaliyofanyika kimkoa kwenye Uwanja wa Jamhuri, mjini hapa.

Muslim alisema kutokana na kukithiri kwa matukio ya mauaji, Jeshi la Polisi limeamua kutenga Alhamisi kila wiki kusikiliza kero za jamii ili kuepusha vishawishi, kuhifadhi hasira na matukio ya mauaji.

Alisema utatuzi wa migogoro mbalimbali ikiwamo ya ardhi, mirathi na ndoa , kwenye familia ni chachu ya kupunguza wanandoa kutalikiana na hata wakati mwingine kufikia hatua ya kuuana.

Kamanda Muslim aliwataka wanawake kutambua kuwa wanaume na wao wanaheshimu jitihada za wanawake kutokana na ukweli kwamba nyuma ya mafanikio ya mwanamume kuna mwanamke.

Mkurugenzi wa Ngaiza Foundation, taasisi inayojishughilisha na masuala ya kijamii, Elizabeth Ngaiza, alisema mwaka 2021 walitatua kero 20 za migogoro ya ndoa na kufanya familia kuendelea kuishi pamoja.

Alisema asasi hiyo inashughulikia utatuzi wa migogoro ya ndoa, mirathi, ardhi na vingine kwa jamii na kwamba imefanikiwa kutatua kero hizo kati ya nyingi alizopokea na kuzimaliza.

Hata hivyo, aliwataka wanawake kuacha kufanya viburi kwa waume zao, hivyo kutokuwa chanzo cha migogoro katika ndoa.

"Wako baadhi ya wanawake ambao huanzisha ugomvi kwa waume zao na wakishauona umekuwa mkubwa, hukimbilia kwenye vyombo vya utetezi. Hilo jambo si zuri, kaeni mtunze na kulinda familia zenu," alisema.

Naye mtaalamu wa magonjwa kutoka kituo cha kupunguza ukatili wa kijinsia cha Mkono kwa Mkono, kinachotoa ushauri wa kisheria katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Dk. Elias Mtungilwa, alisema wamejikita katika kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia ili kupunguza na kuzuia ukatili wa kijinsia wa aina zote.

Alisema suala la ukatili wa kijinsia linaweza kupungua kama kutakuwa na ushirikiano mzuri kuanzia kwenye mabaraza ya kata kwa sababu ya uwapo wa baadhi ya wanaofanya ukatili kuwa na nguvu ya kifedha.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala-Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala-Lugala na Nala-Segu kuwa muda wao wa kulipia viwanja hivyo umeisha. Aidha, katika kuwawezesha kukamilisha malipo hayo, amewaongezea muda hadi tarehe 27.03.2022.

Baada ya kukamilika kwa muda huo, viwanja ambavyo vitakuwa bado vinadaiwa vitarudishwa sokoni ili wateja wengine wavinunue bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji, DODOMA**

216731401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bajeti iliyopangwa katika kilimo ifanyike kwa vitendo

**WAZIRI** wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, juzi aliwasilisha sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 huku kukiwa na vipaumbele kadhaa. Moja ya mambo ambayo yalionekana kuleta faraja ni kuwapo kwa nyongeza za mishahara na kupandishwa madaraja kwa watumishi wa umma ambao kwa takriban miaka sita hawakupata haki hiyo.

Katika bajeti hiyo ambayo serikali katika mwaka huo inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 41.06, sawa na ongezeko la asilimia 8.1 kulinganisha na bajeti ya sasa, watumishi wametengewa Sh. trilioni 9.74 kwa ajili ya nyongeza za mishahara na upandishwaji madaraja.

Hatua hiyo ni faraja kubwa kwa watumishi wa umma na ni imani yetu kwamba itaongeza ari katika utendaji kazi na hatimaye kuleta tija na ufanisi. Kwa maneno mengine, bajeti ijayo imeleta faraja kwa watumishi wa umma na kutakuwa na mabadiliko hata katika mzunguko wa fedha kwenye maisha ya kila siku.

Pamoja na watumishi wa umma kukumbukwa, matumaini mengine katika bajeti hiyo ni sekta ya kilimo kupewa kipaumbele cha aina yake tofauti na miaka iliyopita. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kilimo ndio mhimili muhimu katika ukuaji wa uchumi wa taifa.

Taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2020 zinaonyesha kwamba kilimo kina ajiri asilimia 61.5 ya Watanzania wote huku kikichangia asilimia 26.9 ya pato la taifa pamoja na asilimia 65 ya malighafi za viwandani. Sambamba na hiyo, asilimia 59 ya mfumuko wa bei hutokana na hali ya uzalishaji katika kilimo.

Kwa mantiki hiyo, iwapo utekelezaji wa bajeti hiyo utafanyika kwa vitendo, sekta hiyo itasababisha kupatikana kwa ajira nyingi zaidi pamoja na ongezeko la malighafi kwa ajili ya viwanda vya ndani, hivyo kuleta mapinduzi ya kweli katika sekta ya viwanda kupitia Sera ya Tanzania ya Viwanda.

Pia kuwapo kwa maendeleo makubwa katika kilimo kutawezesha taifa kuwa na akiba ya chakula pamoja na ziada ya kuuza nje sambamba na kudhibiti mfumuko wa bei ambao kwa kiwango kikubwa huchangiwa na kupanda wa bidhaa zitokanazo na kilimo.

Hata hivyo, kama ilivyosisitizwa katika eneo hilo, mkazo mkubwa uwe katika sekta ndogo ya kilimo cha umwagiliaji ambayo kwa miaka mingi imekuwa haifanyi vizuri, hivyo kushindwa kuchangia ukuaji wa sekta pamoja na pato la taifa kwa ujumla.

Tanzania imejaliwa kuwa na mito na mabonde mengi ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini eneo linalotumika halifiki hata asilimia 30. Kwa maana hiyo jitihada zinazopaswa kufanyika ili kilimo cha umwagiliaji kilete matokeo makubwa kama ilivyowekewa mkazo katika mipango mingi iliyopita ikiwamo Kilimo Kwanza.

Ili kufikia malengo tarajiwa katika umwagiliaji, serikali kupitia taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) iweke mkazo katika kuwakopesha wakulima wakubwa nyenzo za kisasa ili kuzalisha mazao mengi. Njia nyingine ni kuimarisha ushirikiano wa pamoja kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) mkazo ukiwa kuishirikisha na kuiwezesha sekta binafsi katika utekelezaji wa azma hiyo.

Jambo la msingi ni kuhakikisha yale yanayopangwa yanatekelezwa ikiwamo kutoa fedha katika maeneo yaliyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya kisekta. Tunasema hivyo kwa sababu fedha zinazopangwa kupitia bajeti si zile zinazotolewa. Ni wazi kwamba kama fedha zitatolewa, maendeleo ya kweli katika kila sekta, kilimo kikiwamo, yatapatikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kulikoni ukarabati wa aina hii katika barabara ya lami?

**UJENZI** wa barabara nyingi zikiwamo za mchepuko na za juu jijini Dar es Salaam, umesaidia kupunguza foleni za magari ambazo kwa kiasi fulani zilisababisha watu kuchelewa kufika kwenye shughuli za kila siku.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba kila halmashauri imekuwa ikijitahidi kutenga fedha za kukarabati au kujenga barabara zinazolingana na hadhi ya eneo lenyewe lakini pia kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari.

Kwa sasa karibu kila kitongaji cha jiji hilo kuna barabara za lami na zingine za vumbi ambazo zimechangia kupunguza msongamano .Baadhi ya madereva wakiona msongamano barabara kuu, wanatumia za mchepuko ili kuwahi kule wanakokwenda.

Kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/23, imetenga zaidi Sh. bilioni nne kwa ajili ya kutatua changamoto za barabara ndani ya mamlaka hiyo.

Hiyo ni taarifa ya Mratibu wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) wa Manispaa hiyo, Mhandisi Paul Mhere, aliyoitoa hivi karibuni katika kikao cha kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka 2021/22 na mpango wa mapendekezo ya bajeti ya 2022/23.

Lakini pia barabara za jijini Dar es Salaam kama zilivyo nyingine, huchakaa hivyo kuhitaji kukarabatiwa kwa kufumuliwa upya au kuwekewa viraka vya lami, udongo au changarawe.

Kuharibika au kuchakaa kwa barabara kunaweza kuwa jambo la kawaida na ndivyo mafundi wanaojenga barabara hufanya kwa lengo la kuhakikisha uchakavu unaoweza kusababisha ikiharibika zaidi, hauendelei.

Kabla ya kuendelea zaidi kujadili kile ninachotaka kukizungumzia, nifafanue kuwa mimi si mtaalamu wa masuala ya ujenzi, lakini si vibaya kuelezea kile ambacho ninadhani hakiko sahihi.

Kwa mfano, sehemu ya barabara ya lami inachakaa, halafu mafundi wanakuja wanabandua lami kutoka sehemu hiyo, kisha wanaacha kwa muda mrefu bila kuitengeneza, matokeo yake eneo lililobanduliwa linaendelea kupanuka.

Wakati mwingine mazingira hayo ya kubandua lami na kuacha kwa muda mrefu bila kuweka kiraka, husababisha foleni za magari ambazo si za lazima au hata ajali zinazotokana na madereva kukwepa maeneo hayo.

Ingekuwa vyema wahusika wakatoa ufafanuzi iwapo utaratibu wa kubandua lami sehemu iliyoharibika na kuacha muda mrefu bila kuweka kiraka kama ni sawa au si sawa.

Pamoja na hilo, nimeshuhudia lingine kwenye barabara ya kutoka Segerea kwenda Kinyerezi, jijini Dar es Salaam, ambalo nalo ni la kushangaza au kutokana nami kutokuwa mtalaamu wa ujenzi wa barabara au vinginevyo.

Sehemu ya barabara hiyo imeanza kuchakaa, kiasi kwamba sehemu chakavu zinatakiwa kubanduliwa ili kuweka viraka vya lami, lakini kinachofanyika ni kubandua na kuweka kokoto na kushindilia.

Ufundi huo unaotumiwa na wajenzi hao ndio ambao umenishangaza, kwamba wanaokarabati barabara hiyo wamekosa lami hadi watumie kokoto ambazo hazijachanganywa na lami kuziba viraka hivyo?

Je, uimara wake ukoje, viraka hivyo vinaweza kudumu kwa muda gani? Kwa mtindo huo mashimo yataisha kwenye barabara hiyo kweli kama siyo kuendelea kuacha iharibike zaidi?

Ninadhani kwamba mtindo huo unaweza kuzusha lawama kutoka kwa madereva wa vyomho vya moto kuanzia magari, bajaji na pikipiki wakiamini kuwa ukarabati huo si wa uhakika na unaweza kuharibu vyombo vyao.

Ingawa kokoto hizo hushindiliwa kwenye viraka vya barabara ya lami, siamini kwamba mvua ikinyesha havitazolewa, kwani havijachanganywa na lami ambayo ingesaidia zishikamane, hivyo zinaweza kuzolewa.

Hivi karibuni niliwasikia baadhi ya wakazi wa jijini wanaotumia barabara hiyo tukiwa katika usafiri wa daladala wakiiomba serikali kufutilia mbali ukarabati huo wa kutumia kushindilia kokoto kwenye viraka vya lami.

Madai yao ni kwamba mtindo huo haufai, kwamba hatua hiyo inaweza kusababisha kuongezeka kwa ubovu wa barabara na kuwa chanzo cha kudorora kwa shughuli za kiuchumi na nyingine muhimu, hasa kwa wale wanaotegemea usafiri wa umma.

Wanasema, kero hizo zinaweza kuwakumba pia wenye usafiri binafsi kwa kutumia fedha nyingi kununua vipuri mara kwa mara kutokana na ubovu wa barabara ya lami inayozibwa viraka kwa udongo.

# Waziri abana ma-RC masoko ya machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ameagiza wakuu wa mikoa kuwashirikisha machinga katika kutekeleza agizo la Rais la kuwapanga wafanyabiashara wadogo katika maeneo maalumu.

Bashugwa alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ziara kwenye mradi wa ujenzi wa soko la Machinga unaotekelezwa na Jiji la Dodoma.

Alisema maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kuwapanga wafanyabiashara wadogo katika maeneo maalumu, yanapaswa kutekelezwa bila kuwapo kwa kikwazo chochote.

"Ndugu waandishi wa habari, leo hii tumefanya ziara ya kujifunza katika mradi huu wa soko la wazi la machinga Dodoma unaotekelezwa na Jiji la Dodoma.

Tukiwa pamoja na wakuu wa mikoa yenye majiji, makatibu tawala, wakurugenzi wa majiji pamoja na manispaa ambazo zinaelekea kuwa jiji.

"Lengo la ziara hii ni kujifunza na wao waende kutekeleza kitu kama hiki katika maeneo yao kwani katika eneo hili tunakwenda kuwa na kitu cha kipekee ambacho hakijawahi kuwapo nchini mwetu," alisema Bashungwa.

Alisema kuwa kwa kuzingatia Rais Samia ameshatambua machinga ni sekta rasmi, wakuu wa mikoa wanatakiwa kutekeleza agizo la kuwapanga kwa amani na utulivu.

"Badala ya kwenda nje kujifunza, sasa tumepata eneo ambalo wakuu wa mikoa watalitumia kujifunza katika utekelezaji wa maagizo ya Rais, lakini na sisi viongozi wa mikoa lazima tuwe wabunifu katika kutengeneza miradi ambayo itakuwa na tija kwa machinga na taifa kwa ujumla," aliagiza.

Bashungwa aliongeza kuwa katika kutekeleza miradi ya kuwapanga machinga, Rais alitoa Sh. bilioni tano na tayari Sh. milioni 500 zimepelekwa katika kuongeza nguvu kwenye mradi wa Machinga Open Market Dodoma.

Aliupongeza uongozi wa Jiji la Dodoma ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Antony Mtaka, kwa kubuni mradi huo na kuusimamia kwa kutumia mapato yao ya ndani.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homela, alishukuru kwa ziara hiyo na kuahidi kwenda kufanya marekebisho ya kuboresha miradi ambayo tayari walishaianza katika maeneo yao.

# Wapongeza Mkataba Kimataifa wa Plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kukabiliana na uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na taka za plastiki, Mtandao wa Mkataba wa Kimataifa wa Plastiki umetoa wito kwa nchi mbalimbali, ikiwamo Tanzania, kutambua thamani ya sekta isiyo rasmi, hasa vyama vya waokota taka kama sekta muhimu katika kuondokana na janga hilo.

Kwa mara ya kwanza jukumu la waokota taka limekubaliwa katika azimio la mazingira kama moja ya hatua za maendeleo ya msingi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na taka zitokanazo na bidhaa za plastiki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari, mtandao huo wa mkataba wa kimataifa unawatambua waokota taka hao sio tu kama wadau, bali kama vyanzo muhimu vya maarifa na utaalamu ambao ushiriki wao utakuwa muhimu katika kutatua mgogoro huo wa plastiki.

"Mapema mwezi huu, katika Bunge la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEA), pande zote zilikubaliana juu ya mamlaka ya kujadili mkataba unaofunga kisheria kushughulikia mzunguko kamili wa maisha ya plastiki kutoka kwa uzalishaji hadi utupaji," alisema Mkurugenzi Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Nipe Fagio, Ana Le Rocha, katika taarifa yake hiyo.

Ana alisema kwamba mkataba huo unaonyesha jinsi mzozo wa plastiki unavyoongezeka haraka na jinsi harakati zinazoendeshwa na raia kukabiliana nazo, zimekuwa na nguvu.

"Sasa tuna dhamira ya kimataifa kukomesha uchafuzi wa plastiki," Anna alitamba.

Alifafanua kuwa wanachama wa UNEA walikuwa wamekubali kufanyia kazi mpango huo ambao utatayarishwa na kuidhinishwa katika miaka miwili ijayo na Kamati ya Kimataifa ya Majadiliano (INC).

# Bonite Bottlers Ltd. yatoa ufafanuzi utapeli tangazo la kazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd imetoa ufafanuzi kuhusu tangazo la nafasi za ajira 543 linaloihusisha, ikionya kuwa haijatangaza nafasi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kampuni hiyo, kumekuwa na tangazo linalosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba kampuni hiyo imetangaza ajira hizo kwa vijana wa Kitanzania na kwamba usaili utafanyika mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro mwezi huu.

"Tunapenda kuwafahamisha kuwa taarifa hizi zinazo sambazwa mitandaoni za ajira sio za kweli. Kampuni inayozalisha maji ya Kilimanjaro, Bonite Bottlers Ltd haijatangaza nafasi zozote za kazi.

"Kampuni hutumia vyombo vya habari kama magazeti, redio au ofisi yenyewe kutoa taarifa za kazi au bidhaa zake. Tunaendelea na uchunguzi kubaini chanzo/vyanzo vya taarifa hizi na hatua kali za kisheria zitachukuliwa pindi tutakapobaini wahusika," kampuni hiyo ilifafanua katika tangazo lake la jana.

■**Angalia kwenye tangazo hapo chini kupata taarifa zaidi.**

KILIMANJARO DRINKING WATER

KILIMANJARO DRINKING WATER
P.O.BOX 205 MOSHI INDUSRIAL AREA
KILIMANJARO
TANZANIA.

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA VIJANA WA KITANZANIA**

Kiwanda cha kutengeneza na kuzalisha maji safi na salama ya kunywa **KILIMANJARO DRINKING WATER**. Kinapenda kutangaza nafasi za ajira kwa vijana wa Kitanzania 543.

Kiwanda kimeongeza kasi ya uzalishaji na usambazaji wa bidhaa hadi nje ya mipaka ya Tanzania, hivyo ni wazi kuwa kiwanda kinahitaji Rasilimali watu ili kumudu kasi ya uzalishaji.

**NAFASI ZINAZO HITAJIKA NA SIFA ZA MWOMBAJI.**

1. Wafanya kazi ndani ya kiwanda katika vitengo mbalimbali ikiwemo [illegible]alishaji (**NAFASI 425**)
2. Wahasibu (**Nafasi 22**)
3. Viongozi wasimamizi (**Nafasi 5**)
4. Fundi umeme wa viwandani (**Nafasi 16**)
5. Walinzi (**Nafasi 15**)
6. Wafanya usafi (**Nafasi 10**)
7. Dreva wa magari mak[illegible]wa na ma[illegible]ogo ([illegible]**fasi 25**)
8. Wasambazaji ([illegible]takuwa wana a[illegible]batana na [illegible]dreva ) **Nafasi 25**
9. Mwombaji a[illegible]e raia wa Tanzania m[illegible] [illegible]mri usio pungua miaka 18 na usio zidi miaka 45
10. Mwombaji a[illegible]e na E[illegible]u kuanzia [illegible]idato cha nne na kuendelea

FAKE

Mwombaji aambatanishe n[illegible]kala zake zote (elimu, cheti cha kuzaliwa na leseni) Barua ya maombi ya kazi ikiainisha aina ya kazi anayo omba pamoja na CV.
Maombi ya kazi yatumwe kwenda kwa Afisa Mwajiri (HR) kupitia email hizi. hrkilidrinkingwater@gmail.com au hrkilimanjarowaters@gmail.com
Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **24/03/2022**
Waombaji walio kidhi vigezo tu ndio wata julishwa kuhusu kupokelewa kwa maombi yao

IMETOLEWA NA HR
KILIMANJARO DRINKING WATER

KILIMANJARO DRINKING WATER

KILIMANJARO DRINKING WATER
P.O.BOX 205 MOSHI INDUSRIAL AREA
KILIMANJARO
TANZANIA.

**WITO KWA AJILI YA USAILI**

Ndugu, asante kwa maombi ya kazi, tumezipitia nyaraka zote ulizo tutumia tumejiridhisha kuwa unaweza kutufaa kwa ajili ya kazi; Hivyo tunakuhitaji kwa ajili ya kufanya usaili.

Usaili utafanyika kwa awamu mbili maana bado tunaendelea kuchambua pia maombi yanayo endelea kutumwa hadi mwisho utakapo fika.

Umechaguliwa katika awamu ya kwanza ya usaili ambayo itafayika kwa siku mbili tarehe. **18 & 19/03/2022.**
Usaili utafanyika katika vituo viwili tofauti. Kituo cha kwanza ni ukumbi wa **VETA HOTEL** uliopo **DODOMA** kituo cha pili ni ukumbi wa **NEW CASTLE** uliopo **MOSHI MJINI.**

Kwasababu ya idadi kubwa ya wasailiwa tumeamua kufanya kwa siku mbili mfululizo. Hivyo wote walio chaguliwa kwa ajili ya usaili watatakiwa kuripoti katika kituo cha usaili tarehe **17/03/2022**, hii ni pamoja na wale wanao ishi ndani ya Mkoa wa Dodoma au Moshi.
Kwa siku zote mbili chakula na malazi vitakuwa katika hoteli zilizo andaliwa kwa ajili ya wasailiwa.

Unatakiwa kuthibitisha uwepo wako mapema kwa kulipia pesa kwa ajili ya malazi na chakula ambayo ni **TSH. 35,000/=** kwa siku zote mbili.
Watakao faulu usaili watapewa wiki moja kwenda kujiandaa kisha watatakiwa kuripoti katika kituo cha kazi.

Malipo yatumwe kwa mhasibu kupitia namba **0 657 853 643 MAHAMUDU SIKALUZWE**. Baada ya kufanya malipo tuma majina yako matatu, kituo utakacho fanyia usaili pamoja na sms ya malipo kwenda kwa mhasibu kupitia email hii mhasibukiliwaterdrinks@gmail.com
Watakao shindwa kuthibitisha uwepo wao nafasi zao watapewa watu wengine.

FAKE

IMETOLEWA NA HR
KILIMANJARO DRINKING WATER

## KONA YA UKWELI

# Mbowe aonekane shujaa si msaliti siasa za kiungwana



Na Thobias Mwanakatwe

ILIKUWA Machi 9, 2022 Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alipoamua kwenda katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, kufanya mazungumzo.

Hili lilifanyika ikiwa ni siku moja tu baada ya Mbowe kushiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambapo Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA) liliamua kufanya sherehe hizo mkoani Iringa.

Ninachoweza kusema Mbowe na chama chake sasa wameanza kukoleza moto kuhusu kuwapo kwa siasa za kiungwana na kistaarabu nchini zenye misingi ya kudumisha amani,upendo na mshikamano. Nayasema hayo kwa sababu Mbowe katika mazungumzo yake na Sendiga, alisema ni muhimu kuona siasa zinazofanyika zinakuwa za kistaarabu na zenye upendo na mshikamano badala ya kufanya siasa za ugomvi na uhasama.

Ninavyojua wako baadhi ya watu ndani na nje ya chama chake watamwona Mbowe kama msaliti kutokana na kauli yake hiyo ambayo kimsingi imebadilisha upepo wa kisiasa na kuleta maana na madhumuni halisi ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini.

Alichokifanya Mbowe ni cha kishujaa na hapaswi kuitwa msaliti kwa sababu siasa si ugomvi bali ni kushindana kwa hoja na jambo hili vyama vingine vya siasa vianze kujifunza kutoka CHADEMA.

Mwaka 1992 Tanzania ilipoamua kuingia katika vyama vingi, ililenga kuwa mfumo huu uwe wa aina ya demokrasia ya ushindani wa kisiasa ili kuleta maendeleo katika nchi husika. Naweza kusema uwepo wa mfumo wa vyama vingi ambao sasa umeshatimiza miaka 29, umesaidia kukiangaliza chama kilichoko madarakani.

Itakumbukwa katika miaka ya hivi karibuni, tumekuwa tukishudia kukiukwa kwa misingi ya kuanzishwa kwa vyama vya siasa kutokana na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kutumia vibaya uhuru wao na kuhatarisha usalama wa nchi. Wako baadhi ya wanasiasa na vyama vyao badala ya kusimama katika misingi ya kidemokrasia, wamekuwa ndio wachochezi wakubwa wa vurugu nchini na wengine kuichafua nchi kimataifa kutokana na maslahi yao binafsi.

Chama cha siasa hasa cha upinzani hakina maana kwamba ni lazima kupinga kila kitu. Hapo ndipo tunashuhudia kuwa vyama vya siasa vingi vimepotoka na kuondoka kabisa kwenye mstari wa misingi ya kuanzishwa kwavyo. CHADEMA imeonyesha njia hiyo sasa wakati umefika kwa vyama vingine vya siasa, viongozi wake wahakikishe wanakuwa wazalendo kwa nchi kwa kufanya siasa za kistaarabu ambazo hazitasababisha nchi yetu kuingia katika machafuko.

Nitawashangaa sana wana CHADEMA watakaoanza kujitokeza kumfanyia mizengwe Mbowe ambaye sasa amekuwa shujaa kutangaza siasa za kiungwana na kistaarabu katika nchi yetu. Watakaojitokeza kumpinga Mbowe watambue kuwa kufanya siasa za chuki na usalama kamwe haziwezi kukifikisha chama hicho mbali kwa sababu Watanzania ni watu waungwana na wastaabu ambao hawajazoea mambo ya vurugu. Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, mwaka 2015 alipojiunga na CHADEMA alionya siasa za uanaharakati kuwa hazina afya katika chama hicho maana ukitazama ndio kinakuwa chanzo cha kufanya siasa za chuki na uhasama. Lowassa aliweka wazi kuwa uanaharakati ni mzuri lakini unafika mahali unavuka ngazi katika kitu kingine ambacho ni chama cha siasa.

Nadhani siasa za uanaharakati ambazo ndizo visababishi vya chuki na uhasama baada ya Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe kutangaza msimamo upya wa kufanya siasa za kiungwana na kistaarabu nina imani hata siasa za uanaharakati zitakuwa zimekufa kifo cha mende ndani ya chama hicho.

Ikumbukwe nchi nyingi za kiafrika ambazo zimeingia katika vita, chanzo chake ni wanasiasa ambao hawataki kuzingatia sheria na katiba za nchi zao. Lakini pia siasa za uanaharakati zinatokana na kuwepo kwa utitiri wa vyama vingi vya siasa, ambavyo baadhi havina itikadi wala mwelekeo katika maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla.

Mwishoni mwa mwaka jana nilimsikia Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya akizungumzia suala la kuwa na utitiri wa vyama akasema hakuleti afya katika nchi. Msuya ambaye alikuwa akihojiwa katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na runinga ya ITV, alisema inashangaza kuona Tanzania kuna utitiri wa vyama kati ya 19 na 22 vilivyosajiliwa katika ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini. Kutokana na utitiri huo wa vyama, Msuya alihoji Tanzania hii demokrasia inayotafutwa kwenye vyama 22 ni nini hasa wakati bado kuna sehemu ambazo watu wana njaa, bado kuna sehemu ambazo wabunge wanaomba barabara zijengwe.

Msuya aliongeza kuwa demokrasia anayoiona isiwe na utitri wa vyama vingi vya siasa bali kutafutwe njia ya kuwa na vyama vichache kama vitatu au vinne na isiwe kulazimisha bali wananchi waulizwe kwa kupiga kura na mwisho wa matokeo ya kura itaonekana kuna vyama ambavyo hawavitaki.

Hakupinga mfumo wa vyama vya siasa uliopo kwani aliweka kinagaubaga kwamba anakubali mfumo wa vyama vingi uendelee kuwapo lakini vyama visiwe vingi kiasi hicho.

Mwanasiasa huyo mkongwe licha ya kuwa Waziri Mkuu aliwahi kushika nafasi mbalimbali serikalini, aliwafumbua macho baadhi ya Watazania kuwa mataifa kama Ujerumani, Korea Kusini, Japan, Malaysia na Singapore yamepiga hatua haraka kimaendeleo kutokana na ushirikishaji wa wananchi katika maendeleo lakini si kwa kuwa na utitiri wa vyama.

Naungana na Msuya kwamba utitiri wa vyama hauna maana katika nchi, hivyo tubaki na vyama vichache tu visivyozidi vitano. Sote tumekuwa tulishuhudia baadhi ya vyama vimekuwa vikiibuka tu unapofika wakati wa uchaguzi mkuu lakini kimsingi kabla ya uchaguzi vinakuwa kimya kama havipo.

Kukaa kimya na kuibuka wakati wa uchaguzi, kimsingi huwa kunazua maswali mengi kwa wananchi kwamba vyama hivi kweli vinafahamu fika jukumu lao au vinaibuka wakati wa uchaguzi mkuu kutafuta maslahi fulani?

Tanzania salama iko mikononi mwetu, tuilinde.

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# JINSI YA KUKABILI HUZUNI YA KUONDOKEWA NA MWENZA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

SUALA la kuondokewa na mtu uliyempenda na kumtegemea husababisha huzuni. Huzuni hii isiposhughulikiwa mapema, inaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya na kisaikolojia kama vile shinikizo la damu, maumivu ya kichwa, kiharusi, magonjwa ya akili, kisukari, kukosa usingizi, kupoteza fahamu, kupoteza hamu ya chakula na mwili kudhoofu hata kusababisha kifo. Hiyo ni kwa sababu akili inakuwa imekataa kukubali kuondokewa.

Kutokana na uzito wa kuondokewa, ni muhimu kujua namna ya kukabili huzuni ili kuepuka athari zake na gharama zisizo za lazima. Mada hii imejikita zaidi katika huzuni itokanayo na kuondokewa na mtoto, mwenzi au mzazi kwa njia ya kifo katika familia. Vifo hivi hugusa sana hisia za wanafamilia wengi. Ni kwa mantiki hiyo, ni jambo gumu na mtihani mzito kwa mwanandoa kusema kwaheri kwa mpendwa wake aliyeaga dunia.

Mwanadamu aliyezaliwa, ipo siku atakufa. Katika nyakati hizi, tunashuhudia vifo vya wale tuliowafahamu na ambao hatukuwafahamu. Kwa kuzingatia ukweli kuwa uhai wa mtu ukiondoka hauwezi kurejeshwa, hivyo njia zifuatazo zinamuwezesha mtu kukabili huzuni ya kuondokewa na mwenzi au mtu wa karibu;-

**Fikiri**

Usizuie kufikiri. Kumbukumbu kuhusu marehemu na matukio wakati mlipokuwa pamoja lazima humjia mfiwa. Usiogope fikra zinapokujia. Acha fikra zikujie. Kufikiri ni mchakato ambao humuwezesha mfiwa kukubali kuondokewa.

**Zungumza**

Ongea na watu ambao wako tayari kukusikiliza na siyo wanaokuhukumu.Usisite kuzungumzia tukio lilivyokuwa, kwani kuzungumza husaidia kuondoa machungu (release tension). Kuongea ni mchakato ambao pole pole hupunguza maumivu makali ya kuondokewa.

**Lia**

Kulia ni nafuu tuliyozawadiwa na Mungu wakati mtu anapokuwa katika hali ya mfadhaiko. Usizuie kulia. Usizuie machozi, bali lia na acha machozi yatoke vya kutosha. Machozi ni dawa ya uponyaji wa nafsi. Kulia ni sehemu ya kuachilia hisia za ndani.

Wataalamu wa tiba wanasema, mtu anapofiwa na mpendwa wake, mwili unazalisha kwa wingi kemikali ziitwazo "narcotic" ambazo huondoa machungu. Mwili wa mwanadamu ni mashine inayojikarabati yenyewe. Mtu anapolia, kemikali hizi hutolewa (released) kwa njia ya machozi. Ndio maana ni muhimu kumwacha mtu alie ili atoe machungu aliyonayo katika nafsi.

Hivyo, kulia ni tiba bora sana kuliko vidonge vya usingizi pale mtu anapokuwa ameelemewa na huzuni ya kuondokewa. Kadiri siku zinavyokwenda, kemikali hizi hupungua kwa kuwa machungu nayo huwa yamepungua.

**Changamana na watu**

Ndugu na marafiki ni watu muhimu wakati wa huzuni ya kuondokewa. Kama kuna kipindi kigumu kwa mfiwa yeyote, ni kipindi baada ya mazishi, ambapo waombolezaji wanakuwa wameondoka na mfiwa kubaki peke yake. Hapa ndipo mfiwa anapohitaji sana watu wa kumtembelea ili kumchangamsha, kumfariji na kumtia moyo. Hata hivyo, watu wa kukutembelea wanapokosekana, usijifungie sana ndani, toka na changamana na watu wema.

**Jishughulishe**

Ni muhimu mfiwa afanye shughuli mbalimbali za kuushughulisha mwili baada ya muda wa maombolezo kumalizika, kwani lazima maisha yaendelee baada ya kuondokewa. Katika kufanya shughuli mbalimbali, akili inajielekeza katika shughuli hizo zaidi kuliko msiba, hivyo, kusaidia kuondoa huzuni na majonzi pole pole.

Kufiwa ni hali ya kuhuzunisha (traumatic experience). Ni hali yenye kuleta athari za kiafya na kisaikolojia pale mfiwa anaposhindwa kukabili huzuni; anapokosa faraja na watu wa kumtia moyo. Huzuni ya kuondokewa haitatuliki kwa haraka kwa hiyo ni mchakato wa pole pole.

Huzuni ya kuondokewa huweza kudumu ndani ya mtu kwa kipindi cha kati ya miezi sita hadi miaka miwili au mitatu kutegemeana na mazingira au aina ya kifo. Ni kwa msingi huu, mfiwa huhitaji ushauri nasihi (counselling) ili kumsaidia kukubali hali iliyojitokeza.

Pamoja na kuondokewa, ni muhimu mfiwa amshukuru Mungu. Kushukuru ni tendo ambalo hufuata baada ya mtu kukubali na kupokea kilichotokea. Mawazo ya shukrani huleta uponyaji wa fikra. Kushukuru ni dalili ya ukomavu wa kiimani.

**Liko Tumaini**

Pamoja na kuondokewa, bado lipo tumaini kwamba, Mungu ni upendo kwako na anakuwazia mema siku zote. Jambo la msingi ni wewe kudumisha mahusiano mema na Mungu, kwani yeye ndiye mpaji, tulizo lako la kweli, na mponyaji wa kudumu wa nafsi iliyojeruhiwa na kuumizwa.

Kwa hiyo, usimwazie Mungu kwa ubaya, kwani kuondokewa hakuondoi mamlaka, nafasi na ukuu wake katika maisha yako. Ng'ang'ana na Mungu ili akusaidie kuzikabili changamoto za kuondokewa na kuwa na maisha yenye utulivu na mafanikio.

**■Mch.Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

MACHI 13, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

## Furahia siku na uyoga




Ukurasa 13

## MITINDO

SHINGO DUARA

Fulana zinazomtoa kila mtu




## KATUNIKA

Ukurasa 16





# MWONEKANO MURUA

## Tumia ndizi, asali uone maajabu


Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | E | M | B | E |
| | A | | | O | |
| U | M | A | | N | |
| | B | | I | G | A |
| | I | | | E | |
| J | A | N | G | A | |





## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO


# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
TBC, TOA, SAUMU, DAMPO, SUBIRA, MIHOGO




Alichokifanya Daktari

MTOTO Juma alimtumia ujumbe dada yake kwamba anataka kwenda jijini, Dar es Salaam kutembea kutokana na sifa nzuri anazosimuliwa na rafiki zake.

Dada yake alimjibu Juma kwamba anaweza kwenda, lakini hakuna vitu vizuri kama vya huko kijijini.

Alimwambia kwa mfano kuku anachinjwa Kinondoni, shingo inaliwa Tandale, Kidari Masaki, paja linaliwa Mikocheni, firigisi Magomeni, miguu inapendwa Mbagala, kipapatio kinaliwa Tandika, kichwa Manzese na utumbo Buguruni.

Juma aliposikia sifa hiyo, alimjibu dada yake hawezi kwenda kwa sababu kijijini wanamla kuku wote wao wenyewe.

SWALI

Kuna majiko mawili, sufuria mbili zenye kiasi sawa cha maji na majiko yote yamewashwa kwa viwango sawa. Sufuria ya kwanza ina yai moja, sufuria ya pili ina mayai 15. Majiko yamewashwa muda mmoja. Ni yai moja au mayai 15 ndio yatawahi kuiva?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Marafiki zako kipimo cha hatma mafanikio yako

KARIBU tena msomaji katika sehemu ya pili ya mada yetu iliyopita kuhusu aina za marafiki unaopaswa kuwa nao ili ufanikiwe.

Wiki iliyopita, nilisema si kila mtu ni wa kumsogeza karibu yako. Si kila mtu ni wa kumpeleka nyumbani kwako, hapana! Wako marafiki ambao kazi yao ni kusengenya tu wenzao.

Ni vyema kuwa na rafiki au mtu anayeona mbele, atakayekusaidia na kukupa mawazo mazuri ya biashara. Kwa ujumla, rafiki ni mtu anayependana na kuaminiana na mwingine.

Moja ya mambo makubwa yanayoweza kukuletea mafanikio ni aina ya marafiki au washirika ulio nao. Ukitaka kufahamu hatma ya mafanikio ya mtu yoyote, angalia aina ya marafiki alio nao.

Hebu tuangalie sifa za rafiki bora;-

Kwanza, rafiki mwema ni yule mwenye hofu ya Mungu. Unapokuwa na rafiki wa aina hii, daima atakushauri kumpa Mungu kipaumbele katika mambo yako yote.

Jiepushe na rafiki anayedharau na kupuuza mambo ya Mungu. Rafiki wa aina hii atakushawishi kufanya mambo ya kinyume na mapenzi ya Mungu. Atakufundisha njia za mkato za kufanikiwa nje ya mpango wa Mungu kwa maisha yako.

Mtu unayekuwa naye karibu wakati mwingi inatokea unajikuta kuiga mwenendo wake hata bila yeye kukushawishi. Dunia imejaa watu wanaojuta kwa sababu ya ushirika na marafiki wabaya wasio na hofu ya Mungu.

Pili, rafiki mwema ni yule anayekutia moyo wakati wote. Mara nyingi unapopanga kufanya jambo la maendeleo katika maisha yako, unamshirikisha rafiki yako wa karibu. Kuna marafiki ambao kazi yao kubwa ni kukueleza jinsi ambavyo mpango wako usivyowezekana, kukuonyesha uwezo wako ulivyo mdogo na huwezi kufanikiwa!

Kila ukitaka kwenda mbele, wanakurudisha nyuma ili uendelee kuwa kama wao. Watakueleza jinsi wao walivyoshindwa, jinsi ambavyo hakuna mtu yeyote katika ukoo wenu aliyefanya unalotaka kulifanya akafanikiwa.

Jiepushe kabisa na rafiki au mtu yeyote ambaye kila wakati anakwambia haiwezekani. Usitafute ushauri kwa mtu asiye na tija. Jiulize, atakushaurije wakati maisha yake mwenyewe yamemshinda?

Kama unataka kufanikiwa katika biashara au ndoa huwezi kwenda kutafuta ushauri kwa mtu ambaye ndoa yake imevunjika au biashara yake imefilisika. Ndio, kuna jambo unaloweza kujifunza kutokana na kushindwa kwao lakini siyo kuwataka ushauri!

Marafiki wanaokutia moyo hujiepusha kukulaumu kwani wanatambua kwamba mafanikio huja baada ya makosa mengi. Wanatambua kuteleza siyo kuanguka na wao pia wamepitia hali hizo kabla hawajafanikiwa.

Huwezi kufanikiwa katika maisha kama utaendelea kushirikiana na wakatisha tamaa kwani hatimaye na wewe utakuwa kama wao. Usifuatane na mtu asiyekwenda kokote!

Tatu, rafiki mwema hukudokeza siri ya mafanikio yake. Marafiki wa aina hii ni wachache sana kwani wengi wetu hatupendi wengine wajue tulivyofanya mpaka tukafanikiwa.

Tatizo ni kubwa huku Afrika ukilinganisha na nchi zingine. Hatuko tayari kuwaona wengine wanafanikiwa kwa ushauri wetu. Tunaficha fursa za mafanikio ya wengine hata kama hatuzihitaji. Hatujui kwamba kufanikiwa kwa rafiki yangu ndiyo kufanikiwa kwangu!

Moja ya siri ya maendeleo huko Ulaya ni kule kushirikishana siri za mafanikio na kujikuta nchi nzima imepiga hatua kubwa ya maendeleo. Itakusaidia nini wewe kuwa tajiri aliyezungukwa na maskini katika nchi masikini kwa sababu hutaki kuwashirikisha wengine siri ya mafanikio yako?

Ili kumpata rafiki wa aina hii, mfanye kwanza kuwa mshauri wako (mentor). Rafiki huyu huwa tayari kukulea na kukuimarisha katika huduma au katika maeneo mengine.

Ni vizuri rafiki wa aina hii awe ni yule aliyefanikiwa sana katika eneo ambalo na wewe unatumika humo. Kama ni biashara pata mentor aliyefanikiwa katika eneo hilo, kwenye huduma au masomoni iwe hivyo pia.

Ukiwa karibu na ua la waridi mwishowe hutakosa kupata harufu. Haiwezekani ukawa karibu na watu waliofanikiwa na wewe usipate jambo la kukusaidia.

Mara nyingi inakuwa si rahisi kupata mshauri unayemtaka. Njia mbadala ni kusoma vitabu walivyoandika jinsi walivyofanikiwa.

***Niishie hapa kwa leo. Wiki ijayo tutamalizia sifa mbili za marafiki, kisha umuhimu wa kuwa na marafiki au washirika ili ufanikiwe. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tutumie vita ya Ukraine, Russia kama somo kwa Watanzania

MACHI 8, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia wananchi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, aliutahadharisha umma juu ya uwezekano wa kupanda kwa bei ya bidhaa kutokana na vita vinavyoendelea baina ya Ukraine na Russia.

Alisema lazima kuna bidhaa zitapanda bei kutokana na ukweli kwamba nchi hizo ni wazalishaji wakubwa hasa mafuta na kuwataka wananchi kufanya jitihada za kuhifadhi chakula na kujiandaa kisaikolojia.

Rais alisema wako ambao wanailaumu serikali kuhusu kupanda kwa baadhi ya bidhaa lakini ni nje ya uwezo wao kwa kuwa baadhi ya bidhaa zinatoka nje hasa mafuta ambayo yakipanda yanasababisha bidhaa zingine kupanda.

Katika jitihada za awali, serikali iliondoa Sh. 100 kwenye lita ya petroli na dizeli ili kuwapunguzia wananchi machungu na zilivyotangazwa bei mpya mwezi huu, kulikuwa na ongezeko dogo ambalo lilishapunguzwa makali.

Kwa sasa lita moja ya petroli ni Sh.2,580 kwa Dar es Salaam, huku ikiendelea kupanda kwa kadri ya walikochukulia mafuta yaani mikoani. Iwapo Sh. 100 isingeondolewa, bei ingekuwa ni Sh.2,680 kutokana na kupanda kwa bei hiyo kwenye soko la dunia.

Bidhaa nyingine ambayo imeshindikana kushuka kuwa kwenye mstari wake ni mafuta ya kula hasa ya alizeti, ambayo yameendelea kupaa na kwa vita hii ambayo nchi ya Ukraine ni mzalishaji wa bidhaa hiyo kwa wingi, maana yake haitapatikana tena.

Kwa mazingira hayo, ni lazima kujiandaa kisaikolojia kwa kutumia kwa nidhamu katika hifadhi ya chakula na bidhaa zingine zilizopo, kwa kuwa moja kwa moja kutakuwa na mfumuko wa bei.

Ikiwa mafuta ya petroli na dizeli yatapanda bei moja kwa moja, bidhaa zote hadi chakula zitapanda bei. Hata usafiri nao unaweza kupanda bei kutokana na hali halisi ya bei ya mafuta hadi hali itakapotengamaa.

Ninatambua kuwa biashara ni huria na kwamba serikali inapanga bei elekezi kwenye baadhi ya bidhaa na nyingine ushindani wa soko na upatikanaji wake ndiyo unaamua kupanda ua kushuka kwake.

Wako watakaopandisha kidogo ili kupata faida ya wastani na wako watakaopandisha zaidi ikiwa ndio wenye bidhaa hiyo kwa wingi kuliko wengine.

Tayari kuna baadhi ya bidhaa zimeanza kupanda kwa kisingizio cha ongezeko la bei ya mafuta lakini kimsingi ongezeko hilo si kubwa kuwafanya wapandishe bei kwa kuwa serikali ilishaondoa Sh. 100 kwa kila lita ya mafuta.

Hali hii inatufundisha kama nchi kuanza utaratibu wakujitosheleza kwa kiasi fulani hasa chakula kwa kuwa ardhi yenye rutuba inayofaa kulima mwaka mzima ipo ni namna ya kuitumia tu ili kuzalisha kwa wingi na ziada.

Mathalani, tuna mikoa inayolima alizeti kwa wingi, hivyo ikiwa nguvu itaelekezwa kwenye kilimo hicho, tutaweza kuwa na mafuta ya kutosha na ziada hata kuuza nje ya nchi. Kama baadhi ya nchi zimeweza kuzalisha kwa wingi na kuliteka soko basi hata Tanzania inaweza ikiwa kutakuwa na mipango thabiti na endelevu.

Pia tumeelezwa bidhaa zingine zinazozalishwa na nchi hizo kwa wingi ni ngano ambayo hutumika kutengeneza mikate na vyakula vingine. Kupanda kwake maana yake vitafunwa vitapanda bei na itawagusa wananchi wote.

Natambua kuwa nchini tunalima ngano lakini bado hatujafikia kiwango cha kibiashara, sasa ni wakati wa kuangalia namna ya kuimarisha zao hilo ili tuzalishe kwa wingi kwa ajili ya mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Pia ni muhimu kwa mamlaka za serikali kufuatilia kwa karibu wale wanaopandisha bei za bidhaa holela kwa kusingizia vita, ili kumsaidia mwananchi wa kawaida asiumie kwa ukali wa maisha.

Kuna wakati serikali ilikuja na mkakati wa kufuatilia bei na kutoa maelekezo kwa wafanyabishara, kabla ya utekelezaji limekuja jambo jingine la vita ambalo linaongeza bei ya bidhaa muhimu kama mafuta ambayo yanagusa sekta nyingi kwa upana wake.

Ni muhimu jitihada za kumlinda mwananchi wa kawaida hasa wa kipato cha chini kabisa zikaendelea, kuhakikisha hakuna madhara ya moja kwa moja au makubwa,bali watu waweze kuendelea na maisha.

Lazima kuwe na elimu kwa umma ya namna ya kuhifadhi chakula ili kuachana na utaratibu wa kununua kulingana na mahitaji ya mlo wa muda au siku,wapo wasio na kipato lakini kwa wenye kipato cha kuwawezesha kuwa na akiba ya chakula ni vyema wakafanya hivyo ili kurahisisha maisha.

Tanzania ina wasomi wengi wa masuala ya uhifadhi bora wa chakula. Ikiwa kutakuwa na kampeni muhimu ya kuelimisha umma upo uwezekano wa wananchi wengi kujenga utaratibu wa kuwa na akiba, si kwa ajili ya kukimbia bei lakini kwa manufaa yao nyakati zote.











Sherehe
ya kutimiza mwaka mmoja ya
mtoto Everjoy Emmanuel au anafahamika
kama Mkwakuru Nyapirya Machi 9 mwaka huu,
ilivyofanyika nyumbani kwao Buzuruga
jijini Mwanza.

# MITINDO

Na Christina Mwakangale





# SHINGO DUARA
# Fulana zinazomtoa kila mtu

VAZI la fulana limekuwa maarufu kutokana na sifa zake za kutochagua wajihi wa mtu husika.

Kwa mujibu wa wataalamu wa masula ya mitindo wanasema nguo hizi hazina historia za nchi za kiafrika, chimbuko lake ni nchi za Marekani na Ulaya.

Kutokana na muingiliano wa kijamii, vazi la fulana limekuwa maarufu na kuvuka kuenea duniani kote.

Fulana zimekuwa chaguo la kwanza kwa vijana ambao idadi kubwa hawataki kutumia akili nyingi kuchagua nguo za kuvaa, bali wanataka kuchukua na kuweka mwilini mara moja huku wakionekana vizuri.

Unapouliza kwa nini watu wanapenda kuvaa nguo hizo? Jibu lao ni kwamba ni nyepesi na haichagui aina ya nguo unayotaka kuvaa chini.

**FULANA SHINGO FUPI**

Kwa kawaida fulana mviringo inapendeza kama imebana mwili kiasi na kumfanya mtu kuonyesha umbo lake asili.

Wabunifu wa mitindo wameongeza juhudi ya kuibua mitindo mizuri inayowavutia wateja na kusababisha kuwapo kwa ushindani wa kipekee.

Fulana ya aina hii imetengenezwa ikiwa na shingo yenye umbo la duara, haina kola kama zilivyo aina nyingine. Mikono yake inakuwa mirefu au mifupi, hapo anapewa nafasi mvaaji kufanya chaguo lake.

Fulana mviringo inatengenezwa ikiwa na rangi tofauti, lakini wataalamu wa mavazi wanashauri chaguo zuri ni rangi ya machungwa, nyekundu, nyeupe, bluu na nyeusi.

Je inafaa kuvaliwa na nguo gani? Hakuna shida, fulana mviringo inapendeza kuvaliwa na jinzi au suruali yenye mitindo ya kubana kiasi.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# MWONEKANO MURUA

## Tumia ndizi, asali uone maajabu



KWA kawaida ngozi ya mwanamke inatakiwa iwe laini na yenye unyevunyevu, kwa sababu ni moja ya pambo lake linalomvutia kila mtu.

Wataalamu wa masuala ya ngozi wanasema ngozi laini yenye unyevunyevu ni nzuri kwa sababu huondoa ukavu unaoongeza kasi ya kuzeeka.

Wanashauri si vyema sana kutumia vilainishi vya viwandani kwa kuwa vingi vina kemikali inayoweza kukuathiri. Wanasema kwa kutumia matunda na vitu vya asili ni moja ya njia nzuri ya kuweka ngozi katika uimara na ang'avu.

Baadhi ya matunda ambayo yanapendekezwa kutumia kuboresha ngozi ni ndizi na parachichi.

Lakini ndizi ni tunda lenye faida kubwa kuwa kilainishi kizuri kwenye ngozi na ikitumika vizuri inatoa matokeo mazuri kwa muda mfupi.

MAHITAJI

Jinsi ya kuandaa kilainishi chako unatakiwa kuwa na ndizi zilizoiva,asali kijiko kimoja na chungwa au limao moja.

JINSI YA KUTENGENEZA

Jaribu kupata usaidizi kutoka kwa mtu wako wa karibu kama mwenyewe huwezi, chukua ndizi yako moja, imenye vizuri kisha weka katika chombo chako kisafi.

Weka asali kwenye bakuli uliyoweka ndizi, halafu changanya vizuri na baadae kamua limao au chungwa kwenye mchanganyiko wa ndizi na asali.

Ukimaliza koroga vizuri hadi upate uji mzito ambao utakufanya kujipaka vizuri.

Hatua ya mwisho chukua mchanganyiko wako huo na anza kujipaka mwilini kuanzia usoni, baada ya hapo unatakiwa kukaa kwa muda wa dakika 20, kisha jisafishe kwa maji ya uvuguvugu.

Ili kupata matokeo mazuri unashauriwa kutumia kwa muda wa wiki moja au zaidi.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia siku na uyoga

UYOGA ni mmea wa pekee na wenye maajabu katika lishe.

Wataalam wanasema uyoga ni mmea unaojitegemea, kwani umbo lake, ukuzi, na njia ya kupata chakula ni za ajabu.

Hata hivyo, aina nyingine ni sumu. Jina la kisayansi la uyoga huitwa mycota au mycetes.

Namna ya kupika Uyoga

Uyoga ni mbadala wa nyama kutokana na aina mbalimbali za mapishi utakavyopenda kuupika.

Andaa vitunguu, karoti, uyoga, pilipili hoho, rangi yeyote ile na vitunguu swaumu.

Katakata mboga za majani unazopendelea ambazo umeshaziandaa katika saizi ndogo.

Safisha uyoga wako vizuri na ukate shina kwa chini bila kupasua uyoga na kupoteza umbo lake halisi.

Tengeneza mchuzi rahisi kwa ajili ya kunyunyizia juu ya uyoga wako.

Chukua kitunguu swaumu, mafuta, chumvi na pilipili manga ya unga na changanya na mchuzi wako.

Nyunyuzia mchuzi wako juu ya uyoga ambao tayari umeuandaa.

Tumia kijiko, chota mchuzi na nyunyizia juu ya uyoga kisha weka pembeni kwa saa mbili, acha mchuzi uingie ndani ya uyoga na kuleta ladha nzuri.

Weka uyoga katika oveni au banika kwenye jiko la mkaa kwa dakika nne hadi tano na utakua tayari umeiva.

Wakati uyoga upo jikoni, chukua ule mchanganyiko wa mboga ulizokata weka mafuta kwenye sufuria au kikaango.

Weka vitunguu swaumu kaanga kidogo kisha weka mchanganyiko wa mboga zote zilizobaki.

Kaanga kwa dakika 4 hadi 5 toa katika moto usisahau kunyunyiza chumvi kiasi.

Chukua mchanganyiko wako wa mboga za majani ulizopika na tumia kijiko kuzichota na weka juu ya uyoga wako.

Toa uyoga, weka katika sahani bado ukiwa wa moto.

Hapa tayari unakua ni mlo kamili na unaweza kula na chakula cha aina yoyote kama chipsi, viazi vya kuchemsha, ugali au wali.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Hakikisha nyumba yako inapitisha hewa ya kutosha

## Jinsi ya kuchagua 'Air Freshener'



NDANI ya nyumba au kwenye gari hewa inayoambatana na harufu ya kupendeza ni jambo linalozingatiwa na wengi.
Kwa kutumia 'Air freshener', ni nzuri kutumia katika mazingira hayo na kukifanya chumba chako kuwa na harufu murua ambayo itakuwezesha kukaa kwa muda mrefu bila uchovu.
Hizi ni baadhi ya dondoo ambazo unaweza kuzitumia kuchagua 'Air Freshener' ndani ya nyumba yako.

1: Chagua mashine nzuri ya kutunzia kimiminika chenye mchanganyiko wa harufu nzuri ambayo inaweza kutoa na kuziba katika muda sahihi.
2: Chagua harufu yenye ladha nzuri ya matunda au maua kulingana na wewe unavyopenda.
3: Unaweza kununua freshener ambayo inatumia umeme au kwenye chupa kulingana na uwezo wako, lakini hakikisha ina ubora unaotakiwa.
4: Air Freshener nzuri ni zile zinazowekwa ukutani na zinazotumia kihisia (Sensa) kwani ni rahisi kujiendesha pale hewa itakapokuwa tofauti.

NYUMBA bora ni ile iliyotengenezewa mifumo mizuri ya uingizaji wa hewa ndani. Kwa maana hiyo, nyumba inapokosa mifumo mizuri ya kuingiza hewa, hapo ndipo vichafua hewa ndani huanza kujijenga.

Changamoto kubwa iko zaidi kwenye nyumba za kisasa kutokana na nyingi kuzibwa kila mahali, jambo ambalo limeonekana kuwa la kawaida hasa milango na madirisha yanapokuwa yamefungwa kwa muda mrefu kuliko yanavyofunguliwa.

Njia rahisi ya kuondoa tatizo hili ni kufungua madirisha kila siku pamoja na kuhakikisha nyumba inafanyiwa usafi katika kila njia ya nyumba ambayo ni chanzo cha kuingiza hewa.

Jambo lingine ni kuzingatia usafi wa jumla wa nyumba nzima, kwamba sakafu ziwe safi na zisafishwe kila inapobidi.

Pia inatakiwa kutokuruhusu taka, nguo chafu, vumbi na uchafu mwingine kujijenga kwa sababu kufanya hivyo unakaribisha uwezekano wa kuharibu hali ya hewa ndani ya nyumba.

Unatakiwa pia kutoruhusu vyombo vichafu vijazane kwa muda mrefu bila kusafishwa, na pia kuepuka kuhifadhi nguo chafu kwa muda mrefu bila kufuliwa na kufuta fumbi kila wakati.

Aidha, kama unavyo vifaa vya kisasa vihusianavyo na maboresho ya hewa ya ndani kama vile viyoyozi na feni, hakikisha vinafanyiwa usafi wa mara kwa mara ili chujio zake zisibebe vumbi na kushiriki kulisambaza.

Sababu nyingine inayochangia uwapo wa hewa nzito na chafu ndani ya nyumba ni uvutaji wa sigara ndani. Hilo ni jambo baya ambalo linapaswa kupigwa marufuku kwa kuwa pia linaleta hatari kubwa kiafya.

Hewa hiyo binadamu anahitaji aipate katika kila mahali anapokuwapo iwe ni sehamu pa kazi, nyumbani na kwingineko.

Kutokana na umuhimu huo wa hewa kwa binadamu, nyumbani nako ambako ni mahali muhimu mtu anakotumia muda wake mwingi, kunahitajika kuwe na hewa ya kutosha, si tu hewa lakini pia iwe safi.

Wakati mwingine unaweza ukaingia ndani ya nyumba ukakutana na hewa nzito, ambayo ukikaa muda mfupi unahisi maumivu ya kichwa kwa mbali.


Binadamu tunatofautiana kwa kuwa wako ambao wana uwezo mkubwa wa kuhisi kitu chochote ambacho hakiko sawa kwa haraka ndani ya nyumba hasa upande wa harufu au kunapokosekana hewa nzuri na safi.

Matatizo hayo ya uwapo wa hewa mbaya ndani ya nyumba, yanaweza kuwasababishia wanafamilia matatizo ya kiafya endapo hakutakuwa na ufumbuzi au jitihada za kuweka mazingira ya nyumba kuingiza hewa safi.

Inawezekana mwanzoni likaonekana ni jambo gumu la kufanya ila ni kwamba kuboresha hali ya hewa ya ndani ni rahisi sana. Unachotakiwa ni kuzingatia tu mambo machache na unaweza kuwa na nyumba huru isiyo na harufu na isiyokuwa na vichafua hali ya hewa.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MACHAFUKO KAMA HAYA YANAYOENDELEA DUNIANI NANI ATANI-SHANGAA MIMI KULINDA RASILIMALI ZANGU?
TATIZO UMEJIPA KAZI YA KULINDA BAHARI!
SIKU HIZI UKIJIFANYA KUDAI KISTAARABU UNAKUFA UNAZIKWA DENI UNALIACHA LINA-RANDARANDA DUNIANI 'LINAKUWA YATIMA'
KWANINI UKISHALEWA VIPOMBE VYAKO UNAPENDA KUNI-TAJIA VIJANAMKE VYAKO VYA KILABUNI?
NA WEWE KWA HASIRA UMEONA UJITOE MUHANGA KWA KULIKUMBATIA 'BOMU LA ATOMOKI'
SHEM' KAWA MBOGO KWANI USHAMWAMBIA KAMA USHAMUOLEA MWENZA?
NINGEMWAMBIA UJUE SAA HIZI NAIMBIWA MAPAMBIO... PALE UNAVYO-MUONA KATANIWA NAENDA KUZINDUA KIKOBA CHA KINAMAMA
UMENIKATALIA KUWA, MTOTO WA SHOGA'ANGU SIO WAKO, LEO KUNA VIDUME VIWILI VINATOANA MACHO VINAMGOMBEA..
KWA MAPENZI MKE WANGU KANIPE BUNDUKI YANGU NILIPOIWEKA SIO SALAMA ITALIWA NA PANYA
HAMNA JEMA NYIE, NIKIPITA NJIA ZA PANYA NIKIFANIKIWA MNANISIFU KAMA MALAIKA, LAKINI NIKIKWAMA MTAFUKUA MPAKA MAKABULI YA KWETU!
DEREVA LENYEWE UMELIONA! BAYAAA HALAFU ZEE' MIDEVU KA' BINI LADENI,
JAMANI PUNGUZENI UKALI WA MANENO!
ENZI ZANGU NISHAMKAANGA MAKOFI!
UNAROHO MBAYA TU. KATUWEKE KWENYE FOLENI UONE UTAMU!
KAWAAMBIE WAPANGAJI WAKO NYUMBANI USITUPANGIE SHERIA HUMU
ANABAHATI LEO SIJALEWA NINGEM'BAMANDA MIKOFI PALEPALE KWENYE USUKANI
LILE FOLENI KULE MBELE MBONA LEO MTAFIKA MAKWENU 'LUKWILI'
NNA 'NYAGI' NKUPE?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KUKOGA LAZIMA, KUPAKA MAFUTA MBWEMBWE...

# Russia yalipua uwanja wa ndege, sasa yawekewa vikwazo kila kona



Wingu la moshi likitanda katika mji wa Kyiv baada ya ndege za Russia kushambulia uwanja wa ndege wa kijeshi uliopo mjini humo. **PICHA BBC**

**UWANJA wa ndege wa kijeshi wa Ukraine ulioko kusini mwa mji mkuu wa Kyiv, umeshambuliwa jana kwa kupigwa makombora na ndege za Russia.**

Meya wa Vasylkiv, alisema shambulio hilo liliharibu njia ya ndege na ghala la mafuta, pamoja na kusababisha milipuko katika chumba cha kuhifadhia risasi.

Video iliyotumwa kwenye mitandao ya kijamii, ilionesha moshi mkubwa mweusi ukifuka kutoka kwenye uwanja huo.

Wakati huo huo, mji wa kaskazini uliozingirwa wa Chernihiv ulishuhudia mashambulizi makali ya makombora.

Hakuna huduma ya maji na katika baadhi ya maeneo hakuna umeme.

Bandari ya kusini ya Mykolaiv, ambayo iko kati ya mji unaokaliwa na Russia wa Kherson na mji wa tatu kwa ukubwa nchini Ukraine, Odessa, pia ilishuhudia mashambulizi ya mabomu.

Katika mashambulizi hayo, hospitali ya wagonjwa wa saratani ilipigwa kwa makombora, ingawa ripoti za awali zinaonyesha kuwa haijaharibiwa sana.

Makadirio kutoka kwa maofisa wa ulinzi wa Uingereza ni kwamba vikosi vingi vya Russia viko pembezoni mwa mji mkuu.

Wasiwasi kutoka kwa wakuu wa jeshi ni kwamba wanajiandaa kufanya mashambulizi makubwa zaidi katika jiji hilo na watajaribu kuuzingira pia, kama inavyoonekana katika maeneo mengine kote nchini Ukraine.

Haijawa wazi ikiwa vikosi vya Russia bado vina uwezo wa kufanya hivyo.

Katika hatua nyingine, wakaazi wa mji wa Melitopol nchini humo, wamejitokeza kupinga madai ya kutekwa nyara kwa meya na majeshi ya Russia.

Juzi maofisa wa Ukraine wamechapisha video inayomuonesha meya huyo Ivan Fedorov, akiongozwa akiwa amezibwa macho.Katika ujumbe wake, Rais Volodymyr Zelensky, uliwashutumu Warussia kwa kutumia njia mpya ya ugaidi.

Melitopol, jiji dogo lililoko kusini-mashariki mwa Ukraine, lilikuwa mojawapo ya miji ya kwanza iliyoangushwa na wanajeshi wa Russia.

**RUSSIA YAZIDI KUWEKEWA VIKWAZO**

Marekani na washirika wake wamezidi kuibana Russia baada ya kusitisha uhusiano wa kawaida wa kibiashara na nchi hiyo, huku Rais Joe Biden akiapa kuwa Rais Vladimir Putin, lazima alipe gharama ya uvamizi wake nchini Ukraine.

Ubelgiji na Marekani pia zimetangaza zitakataza mauzo ya bidhaa za anasa kwa Russia katika kile ambacho rais wa halmashauri kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula von der Leyen amekielezea kama pigo la moja kwa moja kwa matajiri wa nchi hiyo.

"Marekani na washirika wetu wanaendelea kuzifunga njia ili kuongeza shinikizo la kiuchumi kwa Putin na kuitenga zaidi Russia katika hatua ya kimataifa," alisema Rais Joe Biden.

Alisema Putin hawezi kuendeleza vita vinavyotishia msingi wa amani na utulivu wa kimataifa na kisha kuomba msaada kutoka kwa jumuiya ya kimataifa.

Rais Biden alionya katika hotuba yake aliyotoa akiwa katika Ikulu ya White House kwamba Putin lazima alipe gharama kama mchokozi katika vita dhidi ya jirani yake.

Kiongozi huyo alitoa hotuba kwa njia ya video katika mkutano wake na rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz na Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, wakijadili mzozo wa Ukraine.

Wabunge wa Marekani ambao ndiyo watakuwa na uamuzi wa mwisho, tayari wameonyesha kuunga mkono Russia kupokonywa hadhi ya upendeleo ambayo inahakikisha kutendewa sawa kati ya washirika wa biashara wa kimataifa.

Katika taarifa iliyotolewa mjini Berlin, viongozi wa G7 walithibitisha kwamba kila mmoja atajitahidi kuchukua hatua ya kuinyima Russia hadhi ya upendeleo wa kibiashara.

Kuiondolea Moscow hadhi hiyo, iliyopatiwa Desemba 2012, kutamruhusu Biden kuzitoza ushuru mkubwa bidhaa za nchi hiyo au kuzuia uagizaji wake.

Rais Biden pia alitangaza kupiga marufuku uagizaji wa vinywaji vikali vya vodka kutoka Russia, almasi na vyakula vya baharini nchini mwake.

Baadaye siku hiyo, wizara ya fedha ya Marekani ilitangaza safu ya vikwazo vipya vinavyolenga wasomi na watendaji wa sekta ya biashara ambao ni washirika na wawezeshaji wa serikali ya Russia.

Vikwazo vya hivi karibuni vinahitimisha duru kadhaa za vikwazo vya kibiashara vinavyokusudiwa kukata uhusiano wa kiuchumi na kifedha wa Russia na mataifa mengine duniani kutokana na uvamizi wake nchini Ukraine.

Hata hivyo, wataalamu wa biashara wana shaka kuhusu kama ushuru mpya utakuwa na ufanisi.

**MAREKANI YAISHUTUMU RUSSIA**

Marekani iliishutumu Russia kwa kutumia mkutano wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kudanganya na kueneza habari za upotoshaji kama sehemu ya uwezekano wa kufanya operesheni ya uongo ili kutumia kemikali au silaha za kibayolojia nchini Ukraine.

Balozi wa Marekani Thomas-Greenfield, alisema Russia ilikuwa ikicheza kile kilichoelezwa katika baraza hilo mwezi uliopita na kuwa atatengeneza madai kuhusu silaha za kemikali au za kibayolojia ili kuhalalisha mashambulizi yake ya kikatili.

"Nia ya uongo huu inaonekana wazi, na inatia wasiwasi sana," alisema.

Aliongeza "Tunaamini kuwa Russia inaweza kutumia kemikali au sumu ya kibayolojia kufanya mauaji, kama sehemu ya tukio la uwongo, au kusaidia operesheni za kimbinu za kijeshi."

Marekani ilionya kuhusu operesheni hizo za Russia sambamba na uvamizi ulioanza Februari 24.

Russia iliomba mkutano huo kushughulikia madai yake ya shughuli za kibayolojia' za Marekani nchini Ukraine, madai yaliyotolewa bila ushahidi wowote na kukanushwa na nchi hiyo.

Ukraine ina mtandao wa maabara za kibiolojia ambao umepata ufadhili na usaidizi wa utafiti kutoka Marekani, lakini zinamilikiwa na zinaendeshwa na Ukraine.

Mtandao huo ni sehemu ya mpango unaoitwa Mpango wa Kupunguza Vitisho vya Kibiolojia ambao unalenga kupunguza uwezekano wa milipuko hatari, iwe ya asili au ya kibinadamu. Juhudi za Marekani zilianza kufanya kazi katika miaka ya 1990 ili kusambaratisha mpango wa zamani wa Umoja wa Kisovieti wa silaha za maangamizi.

Balozi wa China katika Umoja wa Mataifa Zhang Jun alionyesha wasiwasi kuhusu shutuma za Russia na akahimiza uchunguzi ufanyike ili kutoa ufafanuzi wa kina na kukubali uthibitisho.

**UKRAINE YAHOFIA SILAHA KALI**

Balozi wa Ukraine katika UN, Sergiy Kyslytsya, alisema huenda Russia inaandaa operesheni nyingine ya kutisha kwa kuegemea matukio ya uongo.'

Akibainisha kuwa Russia tayari imetumia makombora ya kasi, kurusha roketi nyingi na mashambulizi makubwa ya angani.

"Kwa hiyo ni nini kingine itakachotumia dhidi ya Ukraine ni silaha kali za maangamizi," alisema Kyslytsya.

## MAKALA

# JINSI YA KUTATUA MIGOGORO YA MIRATHI NJE YA MAHAKAMA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

NCHI yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria na mahala sahihi pa kutafsiri hizo sheria ni mahakamani. Lakini katika hali ya kawaida, mahakamani huwa si sehemu nzuri ya kwenda kutatulia matatizo yetu bali huko kunafaa kukimbilia tu iwapo juhudi za mazungumzo ya namna ya kukubaliana zitakuwa zimeshindikana.

Tuna kila sababu ya kupunguza mashauri mbalimbali yasiende mahakamani lakini pia kupunguza idadi ya mahabusu wanaosubiri uamuzi wa kesi zao mahakamani. Kwa hiyo ikiwa zitapatikana njia bora za kukubaliana katika migogoro mbalimbali, tutaweza kuipunguzia serikali gharama za uendeshaji wa kesi na kuwatunza watuhumiwa.

Leo tuangazie kidogo namna bora ya kutatua migogoro ya mirathi nje ya mahakama zetu. Mwaka 2011 tulipata msiba wa baba yetu na wakati wa msiba, baadhi ya ndugu wakaniita pembeni na kunieleza kwamba kwa sababu mimi ndiye kijana mkubwa wa marehemu, nikubali kuandikwa kama mrithi wa mali za baba na sababu yao kubwa ilikuwa kwamba mama aliyeachwa mjane ni mama wa kufikia.

Pamoja na kwamba nilikuwa nawaheshimu sana, nilikataa palepale mpango huo. Sikukataa hivi hivi bali nilitoa sababu kuwa pamoja na kwamba mimi ni kijana mkubwa wa marehemu, pale nyumbani sijawahi kununua hata kijiko. Kwa maana hiyo, nikihitaji mali zangu nitazitafuta mwenyewe, hivyo mrithi wa mali hizo abaki mama yetu. Jambo hili baadhi hawakulipenda na hawakunielewa.

Baada ya hapo, kama ilivyo kawaida wanafamilia, tukakubaliana kwa maandishi kwamba, mrithi halali wa mali za mzee wetu awe mama yetu kama msimamizi mkuu. Ikawa hivyo na tulipomaliza msiba tukarudi nyumbani baadaye tukapeleka muhtasari wa kikao hicho mahakamani kama zilivyo taratibu. Tulipofika mahakamani tukaeleza, basi jambo lile lilimvutia sana Hakimu akataka kufahamu ni kwa namna gani tumefikia uamuzi mzuri kiasi hicho. Hakimu akaniita akaniuliza kwa mara nyingine kwamba ni kweli mama huyu si mama yako wa kukuzaa? Nikasema ndiyo, basi akanambia unawaona wale wamama waliokaa pale (walikuwa wakilia)? Hao wamedhulumiwa mali na ndugu wa marehemu.

Hakimu akatwambia kwa sababu mmekubaliana vizuri sana sisi kama mahakama hatuna haja ya kugawa mali zenu kama sheria inavyotaka, lakini tutakachowasaidia kama mahakama, tutahakikisha mirathi yenu mnaipata mapema iwezekanavyo na kweli ikawa hivyo. Baada ya ushuhuda huo, nije kwenye baadhi ya sababu ambazo zinaweza kuwa chanzo cha migogoro. Moja ni kuhusu uhusiano wetu kama familia. Watu mnapokuwa na uhusiano mzuri katika familia, matatizo yanapotokea ni rahisi kuyatatua. Waliokuwa wananishauri kuhusu nikubali kuwa mrithi hawakuwa wanafahamu jinsi tulivyokuwa na uhusiano mzuri sana na mama yangu.

Ni mama aliyenilea bila kuwa na mtazamo wa kuniona kama mimi ni mtoto wake wa kufikia. Aliniona kama mtoto aliyenizaa nami nilimwona kama mama yangu wa kunizaa. Kwa hiyo sikuona sababu ya kukubali kuwa mrithi wakati mali zote walizitafuta na mumewe (baba). Kuna wakati huhitaji kuwathibitishia watu wanapokuwa na shaka juu yako kwa sababu ukweli hauhitaji kupigiwa kelele. Muda ukifika huwa inaeleweka kwa kila mmoja na leo tutakubaliana kwamba kwa pamoja tulifanya uamuzi wa busara.

Sababu ya pili ni ushirikiano katika kuzitafuta mali zenyewe. Kwanza, tutakubaliana kuwa migogoro ya mirathi waathirika wakubwa ni wanawake (wajane). Sjawahi kusikia kesi za wanaume wakilalamika kwamba ndugu wa mke wamechukua mali zao bali utasikia ndugu wa mume wamechukua mali za ndugu yao na kumwacha mjane na watoto bila kitu. Sasa lazima tujiulize pia kuna nini hapa? Kwa nini kesi nyingi zinawahusu kinamama? Je, ni mfumo dume au ni nini? Hapa kuna mazingira mengi sitaweza kueleza yote lakini kwa mtazamo wangu, kuna mahali panakuwa pengine hapajakaa sawa au mila, desturi pamoja na imani zetu za kidini zInaweza kuwa na mchango katika hili.

Kimsingi, mkishakuwa pamoja kama mke na mume, sheria za kimahakama zinatambua kwamba chochote mnachovuna au kilichokutwa hapo ni chenu wote na maandiko kutoka baadhi ya vitabu vya dini yanasema mmekuwa mwili mmoja. Lakini unapokuja kwenye uhalisia, jamii, marafiki na ndugu wote wanajua kati ya hawa watu wawili nani mwenye mali au nani alikuta nini kwenye nyumba ile na wakati mwingine ndugu walikuwa sehemu ya uwezeshaji wa kupatikana mali hizo kabla ya kuoa au kuolewa. Kwa hiyo inapotokea mmoja amefariki si rahisi ndugu wanaofahamu namna mali hizo zilivyopatikana kukubali mmoja wapo azichukuwe, ikiwa kwa namna yoyote ile wanafahamu hakushiriki katika upatikani wake tayari mgogoro unaanza.

Hapa pia kutokana na mwanya huo wa kisheria, ambao unatambua kwamba mkishakuwa pamoja chako kinakuwa chetu, wako wanawake au wanaume wanaotumia udhaifu huo wa kisheria, yaani unakuwa na mtu kama mume au mke si kwamba unampenda bali unapenda mali zake. Mnaoana baada ya muda unaleta timbwili muachane ukadai talaka ili mali zake iwe sehemu yako au mmoja anafariki dunia uwe mrithi. Hilo nalo linaonekana kuwa sehemu ya tatizo maana ndugu hawatakubali, umekuja leo umekuta mali zipo zaidi ya miaka 20 halafu sheria inakutambua kama mrithi!

Sababu nyingine inaweza kuwa kutokujiandaa kimaisha. Kwenye familia kila mmoja akiwa amejiandaa vizuri kuwa na mali zake, kunapunguza sana migogoro ya mirathi. Inaonekana pia umaskini katika familia zetu unafanya ndugu waanze kung'ang'ania mali za marehemu wakidhani kwamba zitawasaidia kujikwamua kimaisha badala ya kuwaachia watoto wa marehemu ziwasaidie.

Jambo lingine ni imani potofu. Kuna watu wakifariki dunia huwa inaaminika kwamba pengine ameuawa na mkewe au mumewe, hivyo ndugu wa upande wa pili hawawezi kukubali mtu wanayeamini amemuua ndugu yao, arithi mali zake. Wanaona ni bora wazichukuwe kama ni watoto wa ndugu yao walee wenyewe. Hapo mgogoro tayari. Kitu kinachopaswa kufanyika ni moja, kuna haja ya kupitia sheria za umiliki wa mali kwa wanandoa na hii ndiyo sababu ya baadhi ya wanawake au wanaume walio wengi kulazimisha kufunga ndoa haraka ili ndoa iwe tiketi au kibali cha umiliki wa mali za mwenza wake. Sheria hii pia inaweza kutoa mwanya wa mmojawapo kumwahisha (kumdhuru) mwingine kwa sababu anatambua wazi kuwa atakuwa mrithi halali wa mali hizo.

Pili, kila mmoja ajiandae kimaisha ili kutotamani mali za nduguye. Tushirikiane katika kuzitafuta, mwanamke anaweza asiwe na kazi lakini anatakiwa kumjali sana na kumpa moyo mumewe anapokuwa anapitia magumu katika utafutaji. Wako wanaofanya hivyo, lakini wako ambao hawashiriki chochote kwa sababu wanaamini hata ikitokea mume anafariki dunia, yeye ni mrithi halali kwa hiyo hajisumbui.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Marijani na kituko cha mzee Uzegeni



Na Adam Fungamwango

PENDO pendo, si kulazimishana. Pendo pendo, yafaa kulingana." Ni utangulizi wa wimbo uliorekodiwa katikati ya miaka ya 1980 na mwanamuziki mkongwe na maarufu sana nchini hadi leo, Marijani Rajabu.

Aliurekodi wimbo huu akiwa na bendi aliyokuwa akiliongoza ya Dar International.

Ni wimbo wenye kisa cha kushangaza, kufurahisha na kuchekesha kwa jinsi kilivyosimuliwa na kilivyoimbwa, lakini cha kusikitisha kutokana na masahibu yaliyowapata wahusika.

Ni kwa sababu wakati huo nyimbo hazikuwa zikishutiwa video kama sasa. Kama ingekuwa, basi matukio ya wimbo huu yangekuwa kama filamu hivi. Na kwa jinsi Marijani anavyosimuliwa kisa kwenye wimbo huu alioubatiza kwa jina la 'Pendo', hata leo hii inaweza kuchezwa filamu na ikafanya vizuri kwenye soko.

Hiki ni kisa cha wazee wawili marafiki ambao walifikia wakati hadi mmoja kumpa mwenzake binti yake awe mkewe. Inawezekana kuwa si vibaya sana lakini tatizo ni kwamba binti mwenyewe alikuwa hataki.

Ni wimbo wenye mafunzo makubwa kwenye jamii zetu ambayo yataendelea kusimama milele na milele kwa sababu bado watu wataendelea kuoa na kuolewa hadi kiama.

"Uzegeni kamuoza mwanawe kwa rafiki yake mzee Hamisi, sababu Hamisi hajambo kidogo ana nyumba nzuri na kiunga cha minazi." Huu ni ubeti wa pili kwenye wimbo huo wa "Pendo'. Unatuonyesha kuwa kumbe sababu za mzee Uzegeni kumuoza binti yake kwa rafiki yake ni kwa sababu ya mali alizokuwa nazo. Alidhani na yeye atanufaika nazo. Waswahili wanasema uongo ni kuagana. Kama hamkupanga pamoja kuongopa, basi muda mfupi tu uongo hujulikana.

Mzee Uzegeni hapa nadhani 'alizingua'. Angekaa na binti yake na kuyajenga, yote yasingetokea, angeweza kukubali, lakini akamlazimisha.

"Binti Uzegeni kakataa katakata, sababu wote ni wazazi wake, mama yake alipomkubalia, walikula bakora yeye na mtoto wake."

Hapa mzee Uzegeni alitumia mfumo dume. Akalazimisha ndoa kwa lazima. Kwanza binti yake alikataa kwa sababu akiangalia mchumba mwenyewe au mume mtarajiwa umri wake sawa tu na baba yake. Mama yake pia akakubaliana naye. Mzee akaona 'msinitanie', akatembeza bakora ambazo ziliwafanya washushe bendera chini, wakakubali kwa shingo upande.

"Harusi ilibidi ifanyike kwa nguvu, wengine furaha wengine karaha, picha ya harusi binti amenuna mzee anacheka uso umekunjana."

Bahati nzuri tu kwamba wakati huo hakukuwa na 'shooting' ya video, maana ingerekodiwa na kurushwa kwenye mitandao ya kijamii. Ilikuwa kichekesho cha kufa mtu kushuhudia harusi ya aina hiyo.

Kwenye picha tu ya mnato ilikuwa ni kioja. Yaani mzee Hamisi anacheka kwa sababu kaoa, lakini uso umekunjana kwa uzee, binti naye amenuna kwa sababu hajaolewa kwa kupenda, amelazimishwa. Kwa Uzegeni, mzee Hamisi, na baadhi ilikuwa furaha, lakini binti mama yake na ndugu wengine kwao ilikuwa ni harusi ya karaha.

"Harusi imekwisha wamebaki nyumbani hakuna kicheko wala tabasamu. Bi mdogo kachanganyikiwa mzee wake, leo kwenda kumwita 'darling'."

Inabidi tu ucheke. Maana binti kachanganyikiwa, kashaolewa, lakini kila akimtazama mtu aliyemwona zamani alikuwa anamwamkia shikamoo na kumpa heshima zote kama mzee wake, kwa sababu ni rafiki wa baba yake mzazi. Leo tena igeuke amwite mume, hani, bebi, switi duh!

"Vijana wa kiume wakipita mtaani mzee Hamisi tumbo lake joto, kazi kubwa kufunga madirisha na milango yote kupachika komeo. Binti akaona hii tabu gani, ewe Mungu nimekosa nini, siku moja akajiamulia akafanya kila mbinu akaruka ukuta."

Hii ndiyo taabu ya kuona mke ambaye unajua kabisa hakupendi. Mwanamume yeyote akipita, akimsalimia au kuongea naye, unaona kama atakuchukulia. Ndivyo ilivyokuwa na kwa mzee Hamisi, akaanza wivu vijana wakipita. Kitendo cha kufungiwa ndani kama kuku, kikamfanya binti kutoroka.

"Mzee Hamisi akili zikaruka na siku hiyo urafiki ukaisha, karudi mbio kwa Uzegeni, leo leo nirudishiwe pesa zangu. Uzegeni cha kujibu hana na mfukoni senti tano hana, kwenye sherehe alichinja ng'ombe na mdundiko ukakesha siku saba." Ingekuwa sasa tungesema rusha roho, kigodoro, vyote vilikesha. Kumbe pesa zote alizopewa Uzegeni alizitumia kwenye sherehe za harusi. Rafiki yake anadai pesa zake za mahari kwa sababu binti yake kakimbia na hajulikani halipo. Hakuna urafiki tena.

"Usimseme si makosa yake, hakuridhika naye." Unamalizia wimbo huo. Kuna jambo kubwa la kujifunza kwa wazazi kwenye wimbo huu. Ni kutomchaguliwa mtoto mchumba wa kuoa au kuolewa. Hata akiwa mzee, kama mwenyewe ameridhika naye sawa. Lakini kama hataki, hata akiwa kijana, usimpachike mtu asiyempenda kwa sababu yeye ndiye atakayekaa naye siku zote na si wazazi.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-21

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

KESI ya kwanza na aliyetoa hukumu alikuwa Jaji Paul Kilongola wa Mahakama Kuu. Rufani hii sasa ilisikilizwa na Majaji Watatu. Pius Msemwa, Edson Njau na Shaban Jeje.

Ikaanza kusomwa kwanza kwa ufupi na kutambulishwa kuwa ilikuwa rufani ya kesi ya mauaji, Tina Kauzeni, mwenye miaka 18, akituhumiwa kumuua Hafidh Chilambo.

"Mahakama Kuu ilisikiliza kesi ile, ambayo upande wa mashtaka uliongozwa na wakili Heri Seif na mashahidi mbalimbali, akiwamo mke wa marehemu Hellen Kisa, daktari aliyechunguza mwili wa marehemu Thomas Mtuta, pamoja na mfamasia Mwahija Chota." Jaji Jeje aliongea na kuendelea.

Pia ulisikiliza upande wa utetezi, akiwamo mtuhumiwa mwenyewe Tina Kauzeni. Upande wa mashtaka ulithibitisha kwa maelezo ya mdomo na ushahidi wa vielelezo kuwa mtuhumiwa alimuua Hafidh Chilambo kwa kumwekea aina mbili za vidonge kwenye chakula ambavyo vikichangaywa na kuwekwa idadi isiyohitajika inakuwa sumu inayoweza kuumuua mtu kwa saa wili baada ya kunywa.

Kutokana na hilo, Mahakama mbele ya Jaji Kilongola, ilimhukumu mtuhumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Kabla ya siku 30 kupita, upande wa mtuhumiwa ulikata rufani na umewasilisha utetezi kwa ushahidi mbalimbali kwenye Mahakama ya Rufani, hivyo tutaanza kupitia kuanzia leo ili tuangalia kama unaweza kuwa na mashiko au la." Alisema Jaji huyo.

Baada ya hapo mlolongo mzima wa mwenendo wa ushahidi hadi Tina kupatikana na hatia hiyo, ulianza kudadavuliwa, kabla upande wa utetezi kuanza kuwasilisha hoja zao, ushahidi na vielelezo vyao.

Rejea ya ushahidi upande wa mashtaka ukaanza.

Ilikuwa siku ya Ijumaa. Tina Kauzeni aliamka na kufanya kazi zake kama ilivyo siku zote. Ilipofika saa tano asubuhi aliondoka nyumbani hapo. Alirejea baada ya kupita saa nzima. Ilipofika saa nane aliondoka tena nyumbani hapo kwa tajiri yake Hafidh Chilambo. Safari hii alitumia saa mbili. Alirejea nyumbani saa 10:00 jioni.




**Kabla ya mazishi, daktari Thomas Mtuta aliuchunguza mwili ya marehemu na kugundua kuwa ndani ya chakula alichokula, kuliwekwa aina mbili za dawa baridi ambazo si chungu, lakini zikichanganywa na mtu akinywa kwa kuwekewa kwenye kinywaji, au chakula, basi anaweza kupoteza maisha masaa mawili au matatu baada ya kunywa, na athari zinaanza kuonekana kiasi cha nusu saa tu baada ya kuingia mwilini.**

Majira ya saa 10:15, robo saa baada ya kurejea, Chilambo alirejea nyumbani.

Inasemekana kuwa si kawaida sana ya Tina kuondoka nyumbani. Huondoka kwa nadra sana na hata kutumwa na mabosi wake, yaani baba na mama ilikuwa mara chache sana. Mara nyingi wanaotumwa safari za nje, kwenda madukani, sokoni wakati mwingine ni hausiboi au mlinzi wa getini. Siku hiyo kulikuwa na mlinzi tu, hausiboi alikuwa amepata udhuru, alisafiri kwenda kwao.

Hata hivyo, mahakama iliambiwa kuwa hakutumwa na mtu yoyote yule, alikuwa akiondoka tu mwenyewe jambo ambalo si la kawaida.

Siku ya tukio, mke wa Chilambo, bi Hellen tangu saa nne asubuhi alikuwa ameondoka nyumbani hapo na watoto wake wawili, Prisca na Paul, akiwapeleka kwa shangazi yao Temeke. Siku hiyo hiyo jioni yake, Hellen Chilambo alikuwa amealikwa kwenye sherehe za harusi zilizofanyika kwenye hoteli moja Sinza, Dar es Salaam. Kwa maana hiyo kuanzia saa nne asubuhi, hakuwapo nyumbani hadi alipopata taarifa za kufariki dunia kwa mumewe akiwa kwenye harusi.

Mahakama ikaambiwa kuwa kutokana na kutokuwapo kwa mke wa marehemu, mshtakiwa alipata fursa ya kutekeleza azma yake hiyo kirahisi zaidi.

Chilambo alianza kula chakula hicho saa 11:00 jioni kwa sababu alichelewa kurejea nyumbani na hata alipofika bado kuna vitu vingine alikuwa akivifanya. Baada ya nusu saa alianza kujisikia vibaya, lakini alidhani tumbo tu la kawaida. Chakula hicho kiliandaliwa, kikapikwa na kuwekwa mezani na mshtakiwa Tina Kauzeni.

Hali ilianza kuwa mbaya kadri muda ulivyokuwa unazidi kwenda na alifariki dunia saa 2:00 usiku akiwa amefikishwa kwenye Hospitali ya Mwananyamala.

Ushahidi uliendelea mahakamani ulieleza kuwa uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa Chilambo alifariki dunia baada ya kula chakula ambacho kilikuwa na viashiria vya sumu.

Kabla ya mazishi, daktari Thomas Mtuta aliuchunguza mwili ya marehemu na kugundua kuwa ndani ya chakula alichokula, kuliwekwa aina mbili za dawa baridi ambazo si chungu, lakini zikichanganywa na mtu akinywa kwa kuwekewa kwenye kinywaji, au chakula, basi anaweza kupoteza maisha masaa mawili au matatu baada ya kunywa, na athari zinaanza kuonekana kiasi cha nusu saa tu baada ya kuingia mwilini.

Mshtakiwa mwenyewe alikiri vyote, lakini alijitetea kuwa hakujua kama chakula hicho kina sumu au dawa yoyote iliyowekwa. Alipolizwa kwa nini si yeye wakati siku hiyo alikuwa yuko peke yake kuanzia saa nne asubuhi, alishindwa kujibu.

Mfamasia Mwahija Chota, yeye alikuwa mmoja wa mashahidi upande mashtaka aliiambia mahakama kuwa siku hiyo ambayo inayotajwa kuwa Hafidh Chilambo alifariki dunia kwa kula chakula chenye sumu, Tina alifika kwenye duka na kununua aina mbili za dawa.

Mwahija aliionyesha mahakama daftari lake ambalo huandika dawa ambazo huuza. Aina hizo ni moja ya dawa zilizouzwa siku hiyo. Daftari lilionyesha kuwa ziliuzwa saa tano na robo. Robo saa tu, baada ya muda ambao Tina aliondoka nyumbani.

Ni aina hizo hizo za dawa ambazo daktari Mtuta alisema zilionekana kwenye mwili wa marehemu ulipofanyiwa uchunguzi.

Ushahidi wa daktari Thomas Mtuta na mfamasia Mwahija Chota ndio ulioonekana kwa kiasi kikubwa kumweka matatani zaidi Tina kupata hukumu hiyo.

Sasa ukafika wakati wa upande wa utetezi kutoa ushahidi wao kuonyesha vielelezo vyao ambavyo vinaweza kuonyesha kama Tina huenda hakuwa peke yake kwenye kesi hiyo, alishawishiwa kwa kujua au bila kujua, na nia kubwa ni kumpunguzia angalau adhabu inayomkabili ya kunyongwa hadi kufa.

'Nondo' zilizoletwa mahakamani hapo zilikusanywa na mpelelezi Eddy Kamal na kuwasilishwa kwa wakili Florence Tinga ambaye naye alizipeleka mahakamani hapo kama ushahidi upande wa utetezi.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# DIAMOND AJIULIZA NINI KIMETOKEA KIBA, WEMA



KAMA kawaida yake Diamond Platnumz, hutumia nyimbo kuwasilisha mambo yake yanayomkereketa moyoni, safari hii amemtaja Ali Kiba na Wema Sepetu kama watu wanaomuumiza kichwa.

Kupitia ngoma ya 'Nawaza' inayopatikana kwenye EP yake mpya ya FOA Diamond Platnumz amezungumzia tofauti yake ya kimziki na Alikiba kwa kueleza ni ushamba, ujana na kugombania mashabiki.

Diamond Platnumz amesikika akiimba "Nililowaza leo nishawaza sana mi na Kiba ugomvi kipi, nikagundua ni ushamba na ujana wa kugombania mashabiki".

Pia amemtaja Wema Sepetu, kwa kujiuliza kama penzi lake lingekuwa hai hadi sasa kama angekuwa na pesa au angefulia kutokana na maisha ya kujirusha.

# Nani kamfunga Nuh Mziwanda?

UJUMBE alioutoa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Nuh Mziwanda, umetafsiriwa katika mitizamo tofauti, huku idadi kubwa ikuhusisha penzi lilokufa kati yake na msanii mwenzake Shilole.

Hata hivyo, watu walioweka dhana hiyo hawana uthibitisho, lakini kama si kweli nani aliyemfunga Mziwanda, kiasi ambacho anaomba afunguliwe?

Wiki hii Mziwanda aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kwamba "Sipendi bifu wala ugomvi ndio mana napenda sana amani na kuongea ukweli wa moyo wangu bila kujali mtu mwingine atanichukulia vipi, ila ukiona unataka amani na bado mtu ana vita ya kukudidimiza ujue unaelekea kwenye unyonge na kuonewa huruma kama Ukraine".

"Naomba kanifungue niwe huru tena kama zamani, usinifungie nateseka sana nina familia yangu inanitegemea na sihitaji mapenzi na wewe nahitaji ukanifungue tu".

Ujumbe huo unaonyesha kuwa Mziwanda anateseka kwa jambo linalomsibu na ndio maana akaamua kuweka hadharani kwamba anazidi kuangamia na hivyo afunguliwe apate nafuu.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND AKARIBIA CITY
MANCHESTER City wamejiweka katika nafasi ya kumsajili straika wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### UNITED YAPATA KOCHA
KLABU ya Manchester United ina matumaini kumtaja kocha wao mpya wa kudumu mwishoni mwa Aprili, mwaka huu. ***(Mail)***

### POCHETTINO KUTIMULIWA
KLABU ya Paris St-Germain inajipanga kumfukuza Kocha, Mauricio Pochettino lakini bado haijajulikana kama watafanya hivyo sasa au wanasubiri mwishoni mwa msimu. ***(Times)***

### TIERNEY KUTUA MADRID
REAL Madrid wana mpango wa kumsajili mlinzi wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 24. ***(90Min)***

### LACAZETTE KITAELEWEKA
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema klabu hiyo itafanya uamuzi wa kumpa mkataba mpya straika wao, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 30 mwishoni mwa msimu huu. ***(Talksport)***

### SALAH AWEKA NGUMU
FOWADI wa Liverpool, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29, hana mpango wa kusaini mkataba mpya ambao alipewa Desemba, mwaka jana. Raia huyo wa Misri mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2023 na bado hatima yake haijulikani. ***(Fabrizio Romano - via Star)***

### SALISU ANUKIA NAPOLI
MLINZI wa Southampton, Jan Bednarek mwenye umri wa miaka 25 na Mohammed Salisu (22), wanawaniwa na Napoli ya Italia. ***(Corriere dello Sport - via Daily Echo)***

### VALENCIA YAMTAKA GIL
KLABU ya Valencia wanataka kumbakiza winga wa Tottenham Hotspur, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 21. ***(Star)***

### CHUKWUEMEKA ATAKIWA
ARSENAL wanamnyatia kiungo wa kati wa Aston Villa, Carney Chukwuemeka ambae ana umri wa miaka 18. ***(Evening Standard)***

### MOURINHO AMTAKA XHAKA
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 29 wakati wa kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomercato)***

### DIAZ AGOMBEWA EPL
KLABU ya Brighton inaonekana kuongoza mbio za kumsaka mshambuliaji wa Blackburn Rovers, Ben Brereton Diaz, huku Crystal Palace, Everton, Leeds United na West Ham pia zikimtaka kiungo huyo wa kimataifa wa Chile mwenye umri wa miaka 22. ***(Teamtalk)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LACAZETTE BADO HAJAFANYA UAMUZI

**Arteta asema mbivu na mbichi kuhusu mshambuliaji huyo zitajulikana ifikapo...**

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta amevunja ukimya na kuthibitisha hatima ya mshambuliaji wake, Alexandre Lacazette kwenye kikosi chake itatatuliwa baadaye mwishoni mwa msimu huu.

Mkataba wa Lacazette unakwenda kumalizika mwisho wa msimu huu na awali kulikuwa na taarifa mshambuliaji huyo alikataa ofa ambayo klabu hiyo ilimpatia.

Kwa sasa kuna taarifa Lacazette anafanya mazungumzo na klabu yake ya zamani ya Lyon ili aweze kurejea baada ya kuwa huru mwisho wa msimu huu.

Arteta leo anawakaribisha Leicester City kwenye dimba la Emirates katika mchezo wa Ligi Kuu England na wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo, alitoa neno kuhusu hatima ya Lacazette.

"Tumezungumza kwamba mwisho wa msimu, ndio tutakapojua tupo wapi na wapi tunakwenda, kufanya uamuzi wa pamoja," alisema.

"Tumekubaliana kufanya uamuzi mwisho wa msimu, hilo ndio la kuzungumza kwa sasa."

Arteta hakutaka kwenda moja kwa moja , inaweza kuwa nafasi ambayo watashika kwenye msimamo wa ligi, ndio itaamua hatima ya Lacazette.


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
LEICESTER
1 | 1.57
X | 4.27
2 | 5.31

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: SALAH AACHIWA KUAMUA HATIMA YAKE



**LIVERPOOL, England**

KUMEKUWA na minong'ono miongoni mwa mashabiki wa Liverpool kuhusu mkataba wa Mohamed Salah, na kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ametoa neno kwa mara nyingine.

Klopp amesisitiza kama klabu, hakuna la zaidi wanaloweza kulifanya hadi walipofikia kwa sasa.

Kwa hiyo, hali ilivyo, ni suala la Salah mwenyewe kuamua anachokitaka katika majaliwa yake ya kuendelea kucheza klabuni hapo.

Inasemekana Liverpool wameshaweka mkataba mpya mezani na wanachosubiri ni jibu la Salah ambaye hadi sasa, hajasema chochote.

Hii inazua sintofahamu miongoni mwa mashabiki wa klabu hiyo ambao wanamhusudu mchezaji huyo ambaye ni sehemu kubwa ya mafanikio waliyoyapata hivi karibuni.

"Na Klopp alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu majaliwa ya Salah, alikuwa na jibu rahisi tu; "Yeye ndiye mwenye uamuzi."

"Sisi kama klabu tulishafanya kila kinachowezekana, hivyo kilichobaki ni uamuzi wake Mohamed Salah mwenyewe."

# Tajiri wa PSG kikaangoni Uefa

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa PSG, Nasser Al-Khelaifi na Mkurugenzi wake, Leonardo wamefikishwa kwenye Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), kwa uchunguzi baada ya kufanya fujo na kuingia kwenye vyumba vya waamuzi vya kubadilishia nguo bila utaratibu.

Vyanzo vinathibitisha Al-Khelaifi na Leonardo walishuka chini kutoka kwenye sehemu zao baada ya mchezo kumalizika na kwenda katika vyumba vya waamuzi na kuanza kulalamikia uamuzi wao kwenye mchezo ambao walipoteza kwa kufungwa mabao 3-1 dhidi ya Real Madrid.

Kipigo hicho kilizima ndoto yao ya kuwania ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kutupwa nje hatua ya 16 bora.

"Utaratibu umejikita zaidi kwenye kanuni za UEFA ambazo zinahusu msingi mzima wa uendeshaji pia tabia zisizo sahihi za wachezaji na wasimamizi," alisema msemaji UEFA akizungumzana waandishi wa habari.

Malalamiko yao makubwa yalikuwa kuhusu bao la kwanza ambalo alifunga mshambuliaji, Karim Benzema, kuwa kipa Gianluigi Donnarumma alifanyiwa madhambi na ilipaswa iwe adhabu ndogo.

Kocha wa timu hiyo Mauricio Pochettino kwenye kikao na waandishi baada mechi alinukuliwa akisema, "ilikuwa faulo ya wazi na niliwaacha wachezaji wajisikie ile hali ya kutotendewa haki."



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# PAWASA AITAHADHARISHA SIMBA IKIIKABILI BERKANE

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni, Boniface Pawasa, amesema mchezo wa kimataifa wa Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Simba dhidi ya RS Berkane utakaochezwa leo utakuwa mgumu kwa timu zote mbili.

Simba inaikaribisha RS Berkane katika mechi ya Kundi D ya michuano hiyo ya kimataifa itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Pawasa aliliambia gazeti hili jana mechi hiyo itakuwa na ushindani kutokana na aina ya timu zinazokutana kuwa na wachezaji wazoefu na wenye viwango vizuri.

Hata hivyo beki huyo wa zamani wa Simba alisema wenyeji wa asilimia kubwa ya kupata pointi tatu katika mchezo huo na kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele kutokana na rekodi nzuri wanayokuwa nayo wanapocheza nyumbani.

"Katika mchezo uliopita kipindi cha kwanza kocha hakupanga kikosi vizuri na ilisababisha timu ishindwe kufanya vyema, kipindi cha pili walifanya vizuri kwa kuwa alibadilisha mfumo, sasa tunataka atumie mfumo wa kipindi cha pili," alisema Pawasa.

Nyota huyo aliyewahi kuitumikia APR ya Rwanda aliwataka Watanzania waachane na siasa za mpira na badala yake waungane pamoja kuisapoti Simba ambayo inawakilisha bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

Alisema anasikitishwa na vitendo vinavyofanywa na mashabiki kwa nyakati tofauti vya kupigana na kuchaniana nguo na kudai vitendo hivyo visipochukuliwa hatua vitaleta madhara makubwa hapo baadaye.

Aliongeza RS Berkane ni timu inayocheza kimahesabu kutokana na kufundishwa na kocha mzoefu na anayejua kusoma wapinzani.

"Berkane ni timu kubwa na ngumu lakini nina imani Simba wakipambana inafungika, Watanzania tujitokeze kuisapoti timu yetu kwa sababu inapeperusha bendera ya nchi kwenye michuano hiyo," Pawasa alisema.

Simba itashuka dimbani kesho ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa mjini Berkane Februari 27, mwaka huu



Straika wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), Aisha Mnuka (kushoto), akiwania mpira dhidi ya Christer Bahera katika mazoezi ya kujiandaa kurudiana na Botswana ifikapo Machi 20, mwaka huu jijini Gaborone. **PICHA: TFF.**

# Mkandala ageuka lulu Bara

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuonyesha kiwango kizuri katika mechi dhidi ya Simba, kuna tetesi klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zimeanza mchakato wa kumsajili kiungo mshambuliaji wa Dodoma Jiji, Cleophace Mkandala, imefahamika.

Mkandala amebakiza miezi mitatu tu katika mkataba wake wa sasa na klabu hiyo ya jijini Dodoma.

Mkandala alifanikiwa kuwafunika viungo wa Simba na kuwachachafya mabeki wake katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Machi 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, meneja wa mchezaji huyo Kelvin Ferdinand aliliambia gazeti hili hajapokea ofa yoyote si kutoka katika timu yoyote ikiwamo klabu anayoitumikia ya Dodoma Jiji.

"Alisaini mkataba wa miaka miwili, alitumikia mmoja na sasa anamalizia, amebakisha miezi mitatu na hatujapata ofa yoyote kutoka nje ya nchi, ndani ya nchi, hata klabu yake yenyewe Dodoma Jiji bado haijakaa na sisi kuangalia kama wanaweza kuongeza mkataba," alisema Ferdinand.

Taarifa za ndani zinasema mara baada ya mechi hiyo dhidi ya mabingwa watetezi, viongozi wa Simba walionekana kuvutiwa naye na kuonyesha kutaka kumsajili huku Yanga, Azam, KMC na Namungo FC pia zikionyesha kuvutiwa na mchezaji huyo.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 13/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1811 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.71 | 3.16 | 2.57 |
| 14:00 | 5139 | FK Khimki vs Sochi | 3.68 | 3.44 | 1.93 |
| 14:15 | 5462 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 14:30 | 5435 | Fiorentina vs Bologna | 1.64 | 4.01 | 5.02 |
| 15:00 | 3652 | Paris St Germain vs Bordeaux | 1.17 | 7.02 | 14.54 |
| 15:00 | 4824 | Luton Town vs QPR | 2.18 | 3.20 | 3.25 |
| 15:30 | 4940 | Motherwell vs Hibernian | 2.76 | 3.15 | 2.38 |
| 16:00 | 1856 | Basaksehir vs Antalyaspor | 1.76 | 3.56 | 4.44 |
| 16:00 | 2940 | Rayo Vallecano vs Sevilla FC | 3.31 | 3.11 | 2.29 |
| 16:00 | 4072 | Randers vs Silkeborg | 2.77 | 3.36 | 2.40 |
| 16:00 | 4237 | Adana Demirspor vs Sivasspor | 1.93 | 3.45 | 3.74 |
| 16:15 | 4702 | Lausanne-Sport vs BSC Young Boys | 6.11 | 4.73 | 1.43 |
| 16:30 | 1388 | Heracles Almelo vs Vitesse Arnhem | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 16:30 | 1576 | Utrecht vs PSV Eindhoven | 3.68 | 3.63 | 1.88 |
| 16:30 | 3540 | Kryliya Sovetov vs Zenit St Petersburg | 5.68 | 4.31 | 1.49 |
| 17:00 | 1078 | Leeds vs Norwich City | 1.58 | 4.29 | 5.19 |
| 17:00 | 1408 | Angers vs Reims | 2.30 | 2.99 | 3.39 |
| 17:00 | 2122 | Clermont Foot vs Lorient | 2.30 | 3.08 | 3.28 |
| 17:00 | 2204 | Chelsea vs Newcastle | 1.33 | 5.19 | 8.78 |
| 17:00 | 3827 | Strasbourg vs Monaco | 2.48 | 3.18 | 2.88 |
| 17:00 | 3829 | West Ham vs Aston Villa | 2.21 | 3.35 | 3.25 |
| 17:00 | 4391 | Everton vs Wolverhampton | 2.28 | 3.20 | 3.25 |
| 17:00 | 4622 | Southampton vs Watford | 1.61 | 4.09 | 5.19 |
| 17:00 | 5346 | Metz vs Lens | 3.68 | 3.33 | 2.03 |
| 17:00 | 5619 | Verona vs Napoli | 3.36 | 3.46 | 2.11 |
| 17:30 | 5854 | Bayer Leverkusen vs FC Koln | 1.60 | 4.38 | 4.68 |
| 18:00 | 1519 | Racing Genk vs St Truiden | 1.46 | 4.42 | 6.08 |
| 18:00 | 5904 | Brondby vs Aarhus | 1.92 | 3.36 | 3.90 |
| 18:15 | 4025 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.28 | 3.30 | 3.15 |
| 19:00 | 1917 | Spartak Moscow vs FC Krasnodar | 1.64 | 4.12 | 4.41 |
| 19:00 | 2753 | Dundee FC vs Rangers | 8.26 | 4.80 | 1.30 |
| 19:05 | 4660 | Lyon vs Rennes | 2.08 | 3.52 | 3.32 |
| 19:30 | 1385 | Arsenal vs Leicester | 1.57 | 4.27 | 5.31 |
| 19:30 | 2327 | Borussia Dortmund vs Arminia Bielefeld | 1.26 | 6.00 | 9.60 |
| 19:30 | 4384 | Eintracht Frankfurt vs VfL Bochum | 1.88 | 3.63 | 3.88 |
| 20:00 | 2537 | Atalanta vs Genoa | 1.34 | 5.01 | 8.62 |
| 20:00 | 3769 | Midtjylland vs Copenhagen | 2.36 | 3.31 | 2.86 |
| 20:00 | 5713 | Udinese vs Roma | 3.20 | 3.35 | 2.22 |
| 20:30 | 3665 | Kfco Wilrijk vs KAA Gent | 5.92 | 4.44 | 1.47 |
| 20:30 | 5905 | Real Sociedad vs Alaves | 1.51 | 4.11 | 6.41 |
| 21:00 | 1027 | Porto vs Tondela | 1.10 | 8.28 | 20.70 |
| 21:30 | 4978 | Greuther Furth vs RB Leipzig | 7.94 | 5.36 | 1.33 |
| 22:00 | 3726 | AZ Alkmaar vs Twente | 1.57 | 3.83 | 5.50 |
| 22:10 | 2253 | Molde vs Odd Ballklubb | 1.35 | 4.54 | 7.15 |
| 22:45 | 1905 | Torino vs Inter | 4.70 | 3.90 | 1.69 |
| 22:45 | 5270 | Brest vs Marseille | 3.35 | 3.40 | 2.12 |
| 23:00 | 5134 | Barcelona vs Osasuna | 1.40 | 4.62 | 7.77 |
| 23:00 | 5218 | Standard Liege vs RFC Seraing | 1.78 | 3.70 | 4.14 |
| 23:30 | 1769 | Sporting Braga vs Gil Vicente | 1.78 | 3.60 | 4.24 |
| 23:30 | 3244 | Atlanta United FC vs Charlotte FC | 1.65 | 4.09 | 4.79 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Machi 13, 2022
Nipashe




Lacazette bado hajafanya uamuzi

HABARI UK 21

# SIMBA YAKAMILISHA RAMANI YA USHINDI

## Yawaita mashabiki wake kwa Mkapa na kuahidi hawatawaangusha katika...

**Na Saada Akida**

TUMETIMIA. Hiyo ni kauli ya wawakilishi pekee wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa, Simba kuelekea mchezo wao wa Kundi D wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane kutoka Morocco, utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo itaanza saa 10:00 jioni kwa saa za Tanzania wakati mchezo mwingine wa kundi hilo utawakutanisha Asec Mimosas ya Ivory Coast dhidi ya US Gendarmerie ya Niger ambao utachezwa kuanzia saa 1:00 usiku.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco aliliambia gazeti hili kazi yake alishamaliza mapema katika mazoezi ya jana asubuhi ambayo yalikuwa ya nguvu na yenye mbinu za kuhakikisha RS Berkane hawatoki.

Pablo alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo wa marudiano na timu hiyo katika kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu.

Mhispania huyo alisema mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani kwa sababu timu yake ilipoteza ugenini na sasa wako nyumbani watapambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kujiimarisha kwenye msimamo wa kundi lao.

"Tumepoteza mechi yetu ya tatu dhidi ya RS Berkane wakiwa kwao, sasa tuko nyumbani, hatutawaangusha mashabiki wetu kwa sababu tumefanya maandalizi mazuri, tumefanyia kazi mapungufu yetu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita," alisema Pablo.

Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' alisema benchi la ufundi limemaliza majukumu yake na sasa kazi kubwa imebaki kwao kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Beki huyo alisema wataingia katika mchezo wa leo wakiwa wapya na kuhakikisha wanafuata maelekezo waliyopewa ili kutafuta ushindi na si matokeo mengine.

"Tunatambua utakuwa mchezo wenye ushindani mkubwa kwa sababu tulipoteza kwao, tumesahau mechi hiyo na tuko wapya na tayari kuwapa raha mashabiki wetu siku ya kesho (leo), tunawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi, kwa sababu wenzetu walipata sapoti kubwa nyumbani kwao, tunawahakikishia hatuwaangushi kwa kuwapa furaha," alisema beki huyo.

Naye Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo' alisema ana imani kubwa timu yao itafanya vizuri katika mchezo wa leo na hatimaye kujiweka katika nafasi nzuri ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

"Kupoteza mbele ya RS Berkane haitupi presha kwa sababu tuliwahi kufungwa na Al Ahly mabao matano na AS Vita walitufunga mabao matano, lakini tulitinga hatua ya makundi na kufika robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika. Mafanikio siyo kitu chepesi kuna hatua na sisi tunataka kuwa bora," alisema Mo.

Winga wa RS Berkane, Tuisila Kisinda, alisema kikosi chao hakina wasiwasi wala hofu kuelekea mchezo wa leo kwa sababu wanaifahamu vyema Simba.

"Hakuna mchezaji tunayemhofia au atakayetuzuia, tuko tayari kusaka ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri, tunaifahamu Simba na wachezaji wake wote," alisem Kisinda.

RS Berkane yenye pointi sita ndio wanaongoza kundi hilo wakifuatiwa na Simba yenye pointi nne sawa na US Gendarmerie wote wakiwa na pointi nne huku Asec Mimosas ikiburuza mkia kutokana na kujikusanyia pointi tatu pekee.




Pablo Franco

## Yanga, KMC FC katika vita mpya

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI jana ikicheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi Timu ya Taifa ya vijana ya Somalia (U-23), Yanga imesema mchezo huo ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya kujiandaa kuwakabili KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Machi 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wamekuwa makini kufanya maandalizi ya muda mrefu kwa ajili ya mechi zao za Ligi Kuu ili wafikie malengo wanayoyahitaji.

Bumbuli alisema tayari wameshaipeleleza KMC na kwa msingi huo, waliamua kucheza mechi ya kirafiki ili kuimarisha viwango vya wachezaji wake.

"Tunakwenda kwenye mchezo mgumu sana dhidi ya KMC. Ni mchezo wa kiufundi na kimbinu. Kama wengi wanavyotarajia hautokuwa mchezo rahisi na sisi pia tunajua hautokuwa rahisi, lakini kama tulivyosema tangu mwanzo ili tuweze mabingwa msimu huu, basi kila mechi kwetu sisi ni fainali," alisema Bumbuli.

Aliongeza KMC ni timu nzuri kwa sababu imekuwa ikipata matokeo bora, hivyo hawatoingia kwa kubweteka au kuwadharau.

"Tunahitaji pointi tatu kwa KMC na nyingine katika kila mechi inayofuata ili tuwe mabingwa, KMC siyo timu ya kubeza hata kidogo, wamekuwa na matokeo mazuri kwa siku za karibuni, lakini sisi tumekuwa na matokeo mazuri zaidi tangu kuanza kwa msimu huu," kiongozi huyo alisema.

Yanga itakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa inaongoza ligi kwa kuwa na pointi 45, ikiwa pia ndiyo timu iliyofunga mabao mengi mpaka sasa, ikipachika magoli 29, ikifungwa mabao manne ambayo ni machache zaidi kuliko timu yoyote, mbali na yote ni timu pekee ambayo haijapoteza mchezo mpaka sasa.

Vinara hao wameshinda mechi 14 na kutoka sare michezo mitatu wakati katika msimamo wanafuatiwa na mabingwa watetezi, Simba yenye pointi 37.

Ligi Kuu Tanzania Bara itanarajia kuendelea tena keshokutwa kwa Biashara United kuwakaribisha Prisons huku Machi 16, mwaka huu Namungo FC itawaalika Azam FC kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, mkoani Lindi.

9 770856 541002